BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWAKATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2018

# 021 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2018

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ... iv

1.0 UTANGULIZI ... 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ... 1

2.1 SEHEMU A: UFAHAMU ... 2
- 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu ... 2
- 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho ... 6

2.2 SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ... 9
- 2.2.1 Swali la 3: Mjengo wa Tungo na Matumizi ya Kamusi ... 9
- 2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno ... 12
- 2.2.3 Swali la 5: Uambishaji wa Maneno ... 17
- 2.2.4 Swali la 6: Aina za Maneno na Mjengo wa Tungo ... 20
- 2.2.5 Swali la 7: Uundaji wa Maneno ... 23

2.3 SEHEMU C: UANDISHI ... 26
- 2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Barua ... 26
- 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Matangazo ... 31

2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI ... 34
- 2.4.1 Swali la 10: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ... 34

2.5 SEHEMU E: FASIHI KWA UJUMLA ... 39
- 2.5.1 Swali la 11: Uhakiki wa Fasihi Simulizi ... 39
- 2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi ... 43
- 2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya. ... 49
- 2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya ... 55
- 2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Ushairi ... 63

3.0 UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA ... 67

4.0 HITIMISHO ... 67

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ... 69

KIAMBATISHO A ... 70

KIAMBATISHO B ... 71

KIAMBATISHO C ... 72

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania lina furaha kutoa taarifa ya uchambuzi wa majibu na kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2018 kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayotoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani huo. Majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa waliyopata au kushindwa kuyapata katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa ngazi ya elimu ya Kidato cha Nne.

Uwasilishaji wa taarifa hii ya uchambuzi unalenga kutoa sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au vibaya katika mtihani huu. Uchambuzi uliofanyika kwa kila swali umebaini pia mambo yaliyosaidia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa wa mada mbalimbali katika somo, kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Pia, sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa hususani katika kutoa majibu yasiyojitosheleza.

Aidha, sababu zilizofanya watahiniwa kufanya vibaya maswali ni pamoja na kutokuelewa matakwa ya maswali mbalimbali na kukosa maarifa/ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha kuhusu dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kupata ufumbuzi wa kasoro mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii. Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wanafunzi wanaohitimu Kidato cha Nne watapata ujuzi katika kujieleza na kufafanua dhana mbalimbali kwa ufasaha.

Mwisho Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani kwa Maafisa Mitihani, walimu na wadau wengine wa elimu pamoja na wafanyakazi wa Idara ya TEHAMA waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2018 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huu ulikuwa na maswali kumi na tano (15) yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D, na E kwa kuzigatia mada za Ufahamu, Matumizi ya Sarufi, Uandishi, Maendeleo ya Kiswahili pamoja na Fasihi kwa ujumla.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B, na D, swali moja (1) kutoka sehemu C na maswali matatu (3) kutoka sehemu E. Swali la kumi na tano (15) lilikuwa la lazima

Jumla ya watahiniwa 360,403 walitahiniwa katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2018. Kati yao, watahiniwa 320,041 sawa na asilimia 89.32 ya watahiniwa wote walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha kufaulu kwa ujumla ni cha juu kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2017 ambapo, asilimia 84.42 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata daraja A hadi D.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni *vizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri kilikuwa na alama 65 hadi 100 na kiliwakilishwa kwa rangi ya kijani, kiwango cha wastani kilikuwa na alama 30 hadi 64 na kiliwakilishwa kwa rangi ya njano na kiwango hafifu cha kufaulu kilikuwa na alama 0 hadi 29 na kiliwakilishwa kwa rangi nyekundu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na watahiniwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, uchambuzi huu utaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua uchambuzi wa kina kwa kila swali na majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyofanywa vizuri, wastani na yale yaliyofanyika vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa kiwango cha juu, wastani au cha chini kwa wanafunzi zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sambamba na hayo, sampuli za majibu yao kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo.

## 2.1 SEHEMU A: UFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mtahiniwa kuonesha umahiri wa kusoma kifungu cha habari, kujibu maswali aliyopewa na kufanya ufupisho wa kifungu cha habari.

### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 6 na liligawanyika katika vipengele (a) hadi (d). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kueleze kitu kilichoathiri uzuri wa Mwanaheri. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kuandika nahau mbili zinazopatikana katika kifungu cha habari alichokisoma. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kufafanua methali mbili (i) Maji yakimwagika hayazoleki, (ii) Asiyesikia la mkuu huvunjka guu; huku akitoa mifano halisi kutoka katika simulizi aliyoisoma na kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari aliyoisoma.

Watahiniwa 329,630 sawa na asilimia 91.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo asilimia 66.5 sawa na watahiniwa (219,263) walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 161,785 sawa na asilimia 53.4 waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 2 hadi 3.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa

mmoja alieleza katika kipengele (a) kuwa, kitu kilichoathiri uzuri wa Mwanaheri ni *kukosa mtoto* badala ya kuelezea athari iliyotokana na tabia yake ya umalaya; mwingine alishindwa kubainisha nahau mbili zinazopatikana katika kifungu cha habari alichopewa na kisha kupata alama za wastani. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele vya swali hili na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 1.1**

| | |
|---|---|
| 1(a) | Kwa mujibu wa habari niliyosoma kitu kilicho-athiri uzuri wa Mwanaheri ni Mwenendo, Mwenendo huu ulimpa jina baya la kuitwa jamvi la wageni. |
| (b) | - Afae hakosi mzishi<br>- Wamekata mguu |
| (c) | - Maji yakimwagika hayazoleki ina maana ukiitupa bahati haitojirudia tena. Mfano: Mwanaheri alikuwa akijiona yeye ndio yeye.<br>- Asiyesikia la mkuu huvunjika guu ina maana asiyesikia la wazazi wake au la wakubwa zake atakuja kuambulia matatizo. Mfano: Mwanaheri alipoichezea bahati. |
| (d) | ASIYESIKIA LA MKUU HUVUNJIKA GUU. |

**Kielelezo 1.1:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika kipengele (b) (i) na kutoa ufafanuzi usiotosheleza katika kipengele (c).

Watahiniwa 57,478 sawa na 13.1% walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 4.0 hadi 6.0 kwa kuwa walimudu kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili. Watahiniwa hao walizingatia ufahamu wa kifungu cha habari na kuweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Hivyo, waliweza kueleza kitu kilichoathiri uzuri wa Mwanaheri kuwa ni mwenendo au tabia yake ya umalaya; na kuandika nahau mbili zinazopatikana katika habari kuwa ni *jamvi la wageni* na *kata mguu*. Vile vile, walifafanua methali na kutoa mifano halisi kutoka katika habari

waliyosoma kama vile, *maji yakimwagika hayazoleki* ikimaanisha jambo likiharibika halitengenezeki; *asiyesikia la mkuu huvunjika guu* ikimaanisha mwenye kukataa maonyo huishia kujiponza mwenyewe. Pia waliweza kuandika kichwa cha habari kilichofaa kwa habari hiyo kuwa ni "Dunia hadaa ulimwengu shujaa" au "Majuto ni mjukuu". Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kujibu vizuri vipengele (a) hadi (d).

**Kielelezo 1.2**

1 (a) Kitu kilichomuathiri uzuri wa Mwanaheri ni umalaya (uasherati) kipindi alichok alipokuwa kijana kwani hakuwajali wazazi wala viongozi wa dini na hiyo ndiyo ilimfanya awe muhuni zaidi na hatimaye kupoteza nafasi ya ~~kutaputa~~ kupata mtoto

(b) i) Jamvi la wageni
ii) kujitoa kimasomaso

(c) i) Maji yakimwagika hayazoleki, Mwandishi ~~amean~~ amemlenga Mwanaheri kuwa bahati alirudi mara mbili hiyo Mwanaheri alicheza na ujana hakutaka kupata mtoto sasa hawezi kupata mtoto na awezi kurudia katika hali ya mwanzo, tukio likishatokea haliwezi kuzuilika.

ii) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu, yaani mdharau mwiba guu huota tende kwani Mwanaheri alidharau ushauri wa wazazi na viongozi wa dini na hatimaye anaangukia katika matatizo hivyo asiyeelewa ushauri wa watu hatimaye hujutia mwenyewe.

(d) MAJUTO NI MJUKUU.

**Kielelezo 1.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vipengele (a) hadi (d) vizuri na kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 110,367 sawa na asilimia 33.5 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 1.5 kutokana na kutoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele vingi. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kuhusisha kifungu cha habari katika kujibu maswali na wengine, walishindwa kubainisha *methali* na *nahau* zilizotumika katika kifungu cha

habari kwa kubainisha kwa kuzichanganya dhana hizo kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kujibu kipengele (a) hadi (c) kwa kuandika:

> *Katika kipengele (a) alikuwa hapitwi na mwanaume badala ya 'tabia yake ya umalaya', (b) alitumia methali ambazo hazikuwa katika kifungu cha habari mwenzio akinyolewa wewe tia maji na kama hujui kufa tazama kaburi badala ya kubainisha nahau 'jamvi la wageni' na 'kujitoa kimasomaso' (c) alishindwa kufafanua methali mbili alizopewa kwa kuandika methali zisizokuwa katika kifungu cha habari yaani; ukifanya kosa usijutie baadae na asiyesikia ya watu baadae hujutia badala ya kufafanua kama (i) Maji yakimwagika hayazoleki ikimaanisha jambo likiharibika halitengenezeki; (ii) Asiyesikia la mkuu huvunjka guu; ikimaanisha mwenye kukataa maonyo huishia kujiponza mwenyewe.*

Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini kutokana na kushindwa kujibu vipengele vingi vya swali hili.

**Kielelezo 1.3**


1. a) alikuwa hapitwi na Mwanaume.

b) i) Mwenzio akinyolewa we we tia maji

ii) Kama hujui Kufa tazama Kaburi

c) i) Ukifanya kosa usijutie baadaye

mfano: Mwanaheri alikuwa hapitwi na Mwanaume yeyote yule

ii) asiyesikia ya watu baadaye hujutia.

mfano: alichezea ujana wake na Wanaume

d) MWANAHERI ANAJUTA KUCHEZEA UJANA WAKE

**Kielelezo 1.3:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili na kupata alama hafifu.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na katika mada ndogo ya *Ufupisho wa Habar*i na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia maarifa ili kufupisha habari aliyoisoma. Swali lilikuwa na alama (4) na lilimtaka mtahiniwa afupishe habari kwa maneno yasiyopungua mia moja (100).

Swali lilijibiwa na watahiniwa 276,157 sawa na asilimia 76.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwao, watahiniwa 226,328 sawa na asilimia 82 walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2***: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 58.1 sawa na watahiniwa (160,213) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 2.5. Watahiniwa hao waliandika ufupisho usiojitosheleza kwa kutokuzingatia baadhi ya mbinu muhimu kama vile mpangilio wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya alama na vituo, idadi ya maneno, matumizi ya lugha sanifu na kutopotosha kiini cha habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja hakuzingatia matumizi ya alama na vituo na kukosea tahajia za maneno kwa kutoacha nafasi kati ya neno na neno, kwa kuandika *nchiambayo* badala ya "nchi ambayo". Pia mtahiniwa mwingine alifupisha habari bila kuandika kichwa cha habari na kutozingatia idadi ya maneno kwa kuandika maneno (60) badala ya maneno mia moja (100) na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 2.1

ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho usiojitosheleza na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 2.1**

2. Mwanaheri alikuwa binti mzuri sana. Ila kali haribu
Kuzuri wake kwa muenendo wake mbaya. Katika ujana
wake aliishia kutembea na wanaume na kufanya stare
he. Akuwaza kupata mtoto kwani aliona hataharibu starehe zake. Sasa
amezeeka ana mtu wa kumsaidia amebaki tuu anajutia. Rafiki
zake pia wamemkimbia. Ila ndugu zake wachache huja na kum
salimia ama kweli ujana ni maji ya moto.

**Kielelezo 2.1**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutozingatia baadhi ya taratibu za ufupisho wa habari.

Watahiniwa 66,115 sawa na asilimia 23.9 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 3 hadi 4 kutokana na kufuata kanuni na taratibu za ufupisho wa habari ilivyostahili. Watahiniwa hao walizingatia mpango wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya alama na vituo, kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari, idadi ya maneno na matumizi ya lugha sanifu. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho unaokidhi kanuni na taratibu za ufupisho kama inavyotakiwa.

**Kielelezo 2.2**

2. Ufupisho
Katika Ulimwengu wa sasa vijana wengi huona
kama ujana ndio Mwisho wa kila kitu husahau kuna
kuna maisha baada ya ujana na badala yake kufanya
starehe za kila aina na mambo yote yasiyofaa.
Pamoja na Mafunzo yote yanayotolewa na wazee
pamoja na watu mbalimbali lakini bado imekuwa
ugumu kwa vijana hawa kubadilika.
Kama ilivyo kwa Mwanaheri aliona kuwa ujana
ndio mwisho wa Mambo yote katika Ulimwengu
na hakuna chochote kimpasacho kupita pasipo
kujaribu hivyo akasahau athari. Kama unambukizwaji
wa Magonjwa pamoja na ukosefu wa watoto.
Kwa kuwa majuto ni mjukuu naamini kuwa
vijana wote wenye tabia na hulka za Mwanaheri
watakuja kujuta siku moja yakiwafika.

**Kielelezo 2.2:** Sampuli ya jibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kuzingatia taratibu na kanuni za ufupisho na kupata alama za juu.

Watahiniwa 49,829 sawa na asilimia 18 waliofanya swali hili walishindwa kufupisha habari na kupata alama za chini 0 hadi 1. Watahiniwa hao hawakuzingatia taratibu za ufupisho kwa jumla. Baadhi yao kutokana na kukosa maarifa ya kufupisha habari waliyopewa, walitunga habari nyingine zilizohusu tabia na mienendo ya vijana, kuhusu wanawake, amani ya nchi na utoaji mimba kinyume na matakwa ya swali na kupata alama 0. Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufupisha kifungu cha habari kwa kuandika mambo yasiyohusiana na habari aliyopewa.

**Kielelezo 2.3**

2 Hii ndiyo nchi yetu nchi maskini nchi ambayo Wanawake wanaiga mambo yasiyofaa Mavazi wanayo vaa hayafai Wanaweka nywele bandia na kuweka kope bandia
hii ndio nchi yetu nchi ambayo inaamani na utulivu lakini mambo yake yananotendwa nihatari sana Vijana sasa hawaambiliki ukiwa Mbia Mara ech!! sasa niwakati mwingine sio kama zamani Vijanawamo kuwa hawa ambiliki wakiroliwa Swali Chini ya makalio nakujitia mashalo ~~lakini~~ pasipo kujua wana haribikiwa kimaisha
Watoto wakike nao wamo kuwa hawa shikiki hawaambili wa makuwa kama watoto wa punda kwani mambo yanayofanyiwa hayo mpendenzi Mungu wamekuwa wake toa mimba pasipo kumuogopa mungu wala wazazi hii ndiyo nchi ya Amani lakini mambo yake nihatari Sanaa!

**Kielelezo 2.2**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufupisha habari aliyopewa kwa kuandika mambo mbalimbali yanayohusu vijana.

## 2.2 SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano yaliyomtaka mtahiniwa kutumia maarifa kutambua dhana na dhima za aina za maneno, njia za uundaji wa maneno, tabia za maumbo ya maneno, na kutunga sentensi.

### 2.2.1 Swali la 3: Mjengo wa Tungo na Matumizi ya Kamusi

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, mada ndogo ya *Mjengo wa Tungo* na *Matumizi ya Kamusi*. Swali lilikuwa na jumla ya alama (5), lililenga kupima maarifa na lilimtaka mtahiniwa kufafanua dhana alizopewa na kisha kutoa mfano mmoja kwa kila dhana aliyoifafanua.

Watahiniwa 340,349 sawa na asilimia 94.4 walijibu swali hili na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 72.2 sawa na watahiniwa (245,638) walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 3**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 161,115 sawa na asilimia 47.4 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3 kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele katika kufafanua dhana walizopewa na kushindwa kutoa mfano kwa baadhi ya dhana kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kufafanua kipengele (b) dhana ya "kirai" kwa kuandika kuwa ni *sentensi iliyoundwa kwa kiima na kiarifu* badala ya 'kipashio cha kimuundo kisichokuwa na muundo wa kiima na kiarifu'. Pia, katika kipengele (e) dhana ya " kamusi" alishindwa kuifafanua

kuwa ni 'kitabu cha maneno pamoja na maelezo ya maana ya maneno hayo, lakini katika kipengele (a), (c) na (d) aliweza kufafanua kwa kuvitolea maana na mfano kwa kila dhana. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua baadhi ya vipengele kuhusu dhana alizopewa na kuzitolea mfano na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 3.1**


SEHEMU B:
3: (a) Neno ni neno au maneno ambayo huandikwa au kuzungumzwa saahi ya watu wawili.
Mfano: Anakula.
(b) Kirai ni tungo ambayo yenyewe husimama badala ya kiima na kiarifu na huweza kuwa kamili katika sentensi.
Mfano: Dada ni mgonjwa sana
(c) Kishazi ni tungo ambayo yenyewe huwa na kiima na kiarifu ambayo husimama badala ya neno na kivumishi.
Mfano: Yule anasoma kitabu
(d) Sentensi ni tungo ambayo hutamkwa au huandikwa ili iweze kuleta maana iliyokamilika
Mfano: Mwanafunzi wetu njema hapa.
3: (e) Kamusi ni kitabu cha marejeo chenye msamiati uliyo kamili na huandikwa kwa alfabeti na kuleta maana ya maneno.
Mfano: Book: kitabu

**Kielelezo 3.1:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri vipengele (c), (d) na (e) na kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 24.8 sawa na watahiniwa (84,523) walifaulu kwa kiwango cha juu kwa kupata alama za juu 3.5 hadi 5. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana walizopewa na kutoa mifano toshelevu kwa vipengele (a) hadi (e). Kwa mfano, katika kipengele (a), waliweza kuelezea *neno* kuwa ni " kipashio cha lugha ambacho huweza kuundwa kwa silabi moja au zaidi. Pia walitoa mifano ya maneno mbalimbali iliyokidhi maana ya neno; (b) waliweza kufafanua *kirai* kuwa ni "kipengele cha kimuundo chenye neno moja na kuendelea kisichokuwa na

muundo wa kiima na kiarifu", na kutoa mfano sahihi; kipengele (c) walifafanua *kishazi* kuwa ni "tungo yenye kitenzi" na kutoa mfano uliokidhi maana hiyo; (d) walifafanua sentensi kuwa ni *kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili* na (e) walifafanua dhana ya kamusi kuwa ni *kitabu cha maneno pamoja na maelezo ya maana ya maneno hayo* na kutoa mifano ya kamusi kama vile kamusi ya Kiswahili-Kiingereza. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua na kutoa mfano kwa dhana (a) hadi (e) kwa usahihi.

**Kielelezo 3.2**


3 a) Neno ni kipashio cha lugha ambacho huweza kuandikwa kwa silabi moja au zaidi. Mfano wa neno ni Mbwa.

b) Kirai ni mojawapo ya aina ya tungo ambayo haitoi taarifa kamili na mara nyingi hupatikana katika kiima cha sentensi
Mfano wa Kirai ni Baba mkubwa

c) Kishazi hii ni aina ya tungo ambayo huweza kuleta maana au taarifa kamili na pia isiweze kuleta taarifa kamili. Kishazi kikitoa taarifa kamili huitwa sentensi.
Mfano wa Kishazi ni Mtoto aliyeibiwa mkoba

d) Sentensi hii ni aina ya tungo ambayo hutoa maana na taarifa kamili.
Mfano wa sentensi ni Baba analima

e) Kamusi hiki ni kitabu chenye mkusanyiko wa maneno (vitomeo na vidahizo) na maana zake pamoja na jinsi ya kutumia maneno hayo. Kamusi hutoa tafsiri ya maneno yanayopatikana katika lugha fulani.
Mfano wa kamusi ni Kamusi ya Kiswahili Sanifu

**Kielelezo 3.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua neno, kirai, kishazi, sentensi na kamusi kwa usahihi na kutoa mifano iliyokidhi kwa baadhi ya dhana na kupata alama za juu.

Asilimia 27.8 sawa na watahiniwa (94,710) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kufafanua dhana (a) hadi (e) kwa usahihi pamoja na kutoa mifano isiyokidhi dhana hizo. Kwa

mfano, mtahiniwa mmoja alikosa maarifa ya kufafanua dhana za kisarufi alizopewa ambapo katika kipengele (a) alieleza kuwa, *neno huweza kuleta maana tofauti kutokana na neno moja tu ulilosoma*; na kutoa mfano, *asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu*, badala ya kufafanua kuwa neno ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na kuleta maana, kwa mfano; baba, mama, mtoto, mwalimu. Vilevile, katika mtahiniwa huyo alishindwa kufafanua dhana zote katika kipengele (b) – (e), na kutoa mifano isiyo sahihi kama kielelezo Na. 3.3 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 3.3**


3 (a) Neno huweza Kuleta maana tofauti
Kutokana na neno moja tu ulilosoma
mfano asiyefunzwa na mamae hufu
nzwa ulimwengu
(b) Kirai huwezi kutunga sentensi
ambayo haina muundo wa Kiima
wala Kiarifu mfano baba analima
c Kishazi huwezi kuleta maana tofau
Kutokea katika maneno mfano Asha na
Juma
d Sentensi huweza Kuonesha jinsi gani
sentensi zinavyotungwa na kuweza
Kuleta maana inayokubalika.
mfano Jana tumeondoka nyumba
nzima
e Kamusi ni vile vitabu vilivyorojewa
rejewa ili Kuonesha msamiati wa
maneno kutoka jamii ya watu
mfano ~~mame~~ NGOSWE

**Kielelezo 3.3**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua neno, kirai, kishazi, sentensi na kamusi kwa kuandika mambo mseto yasiyofafanua dhana hizo.

### 2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, mada ndogo ya *Mnyambuliko wa Maneno*. Swali lililenga kupima uundaji na lilimtaka mtahiniwa

kunyambua maneno aliyopewa ili kupata maneno mawili zaidi kwa kila neno alilopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 342,977 sawa na asilimia 95.2 ya wote waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Asilimia 81 sawa na watahiniwa (277,968) walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 3**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 261,126 sawa na asilimia 76.1 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 3.5 hadi 5 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu unyambuaji wa maneno wenye lengo la kuzalisha maneno mapya. Watahiniwa hao walinyambua maneno *beba, pokea, rudi, soma, shughuli, sema, penda, heshimu, pigo, pika* na kupata maneno mawili kwa kila neno kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kunyambua maneno aliyopewa kwa usahihi na kupata maneno mawili zaidi kwa kila neno kama kielelezo Na. 4.1 kinavyoonesha.

**Kielelezo 4.1**


4 a) beba
-bebesha
-bebeka
b) Pokea
-Pokelewa
Pokelea
c) Rudi
Rudisha
Rudishwa
d) Soma
Someka
Someana
e) Shughuli
Shughulika
Shughulikiwa
f) Sema
Semeana.
Semwa
g) Penda
Pendeka
Pendana
h) heshimu
heshimiana
heshimika
4 i) Pigo
Pigishwa
Pigwa
J) Pika
Pikika
Pikiana

**Kielelezo 4.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyenyambua maneno (a) hadi (j) vizuri kwa kuzalisha maneno mengine mawili zaidi kwa kila moja na kupata alama za juu.

Watahiniwa 16,842 sawa na asilimia 4.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa hao waliweza kunyambua baadhi ya maneno kwa usahihi lakini walishindwa kwa maneno mengine kutokana na kukosa maarifa mahsusi ya unyambuaji wa maneno. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kunyambua maneno katika vipengele nane kwa kuzalisha neno moja na kushindwa vipengele (e) na (i) na hivyo kupata alama za wastani kama kielelezo Na. 4.2 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 4.2**



4 (a) beba — bebwe
(b) Pokea — Pokelewa
(c) rudi — rudisha
(d) Soma — Somemewa
(e) Shughuli —
(f) Sema — Semea
(g) Penda — Pendwa
(h) heshimu — Heshimiwa
(i) Pigo —
(j) Pika — Pikiwa

**Kielelezo 4.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyenyambua maneno aliyopewa na kupata neno moja zaidi badala ya maneno mawili kwa kila moja kama ilivyotakiwa.

Aidha, watahiniwa wachache 65,009 sawa na asilimia 19 pekee walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama za chini 0 hadi 1 kutokana na kukosa maarifa kuhusu mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno* kwa njia ya unyambuaji. Baadhi ya watahiniwa walifafanua maana za maneno waliyopewa na kubainisha viambishi katika maneno hayo na wengine walitungia sentensi maneno waliyopewa badala ya kuyanyambua ili kupata maneno mawili zaidi kama ilivyotarajiwa katika swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kunyambua vipengele vyote alivyopewa kwa kubainisha maana ya kikamusi kwa baadhi ya maneno na katika maneno mengine akatoa ufafanuzi usioeleweka; majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali na kupata alama 0 kama kielelezo Na. 4.3 kinavyoonesha.

**Kielelezo 4.3**



4. (a.) beba
- Kitu kuondoka nacho
- Kifaa kilicho anguka

(b.) Pokea
- ~~Zawadi~~ mawasiliano baina ya watu wawili
- ~~Sima~~ kitu kutoka kwa mtu

(c) rudi
- kuh kuairisha kwenda sehemu uliyo taka kwenda
- Kulejea sehemu uliyotoka

(d.) Soma
- Kilendo anacho fanya mwanafunzi
- Habari zinazotamkwa na mtu.

(e.) shughuli
- Kazi ambazo zipo nyumbani na ofisini
- Tendo ambalo unatakiwa kutenda.

(f) Sama
- Kulusiwa kuongea jambo
- mazungumzo baina ya watu wawili

4. (g.) Panda
- upando baina ya watu wawili
- Sehemu yenye kuwatia

(h.) heshimu
- Watu wazima na wadogo
- Msimamo wa mtu.

(i.) Pigo
- tendo linalofanywa na binadamu.
- Kuumizwa katika moyo wako.

(j.) Pika
- Inaonyesha sehemu yenyewe.
- Tendo analofanya binadamu wakati wote.

**Kielelezo 4.3:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maana mbili kwa kila neno alilopewa badala ya kunyambua maneno hayo ili kupata maneno mawili zaidi.

### 2.2.3 Swali la 5: Uambishaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, mada ndogo ya *Uambishaji wa Maneno* na lilikuwa na jumla ya alama 5. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kubainisha tabia za maumbo yaliyokolezwa wino katika vitenzi alivyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 276,434 sawa na asilimia 76.7 ya wote waliofanya mtihani huu, ambapo watahiniwa 93,177 sawa na asilimia 33.7 pekee walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani na kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha chini cha kufaulu kwa watahiniwa. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 5**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 183,257 sawa na asilimia 66.3 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama za chini 0 hadi 1. Watahiniwa hao walishindwa kubainisha tabia za maumbo yaliyokolezwa wino katika vitenzi walivyopewa kutokana na kukosa maarifa mahsusi katika kubainisha tabia za maumbo ya vitenzi hivyo kama ambavyo walitakiwa kubainisha katika kipengele (a) kuamuru/amri, (b) ukanushi/nafsi ya pili umoja, (c) mtendwa/nafsi ya kwanza wingi, (d) hali ya mazoea, (e) kitenzi kishirikishi (f) urejeshi wa mtenda (g) kitendwa/wingi, (h) kauli ya utendwa na (e) kauli ya utendeka. Watahiniwa hao walikabiliwa na tatizo la kuchanganya tabia za maumbo mbalimbali ya vitenzi walivyopewa na kazi za viambishi katika vitenzi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kubainisha tabia za maumbo

katika vitenzi alivyopewa kwa kuonesha kuwa maumbo yote ya vitenzi hivyo ni njeo za wakati tofauti tofauti kama kielelezo Na. 5.1 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 5.1**


5 a) futa – njeo wakati uliopo umoja.
b) thi – njeo wakati uliopita
c) tu – njeo wakati uliopo wingi
d) hu – kauli ya kutenda.
e) ni – kiulizi
5 f) ji – wakati uliopo katika umoja.
g) Vi – njeo wakati uliopita wingi
h) kwa – njeo wakati uliopita
i) -ika – wakati uliopita

**Kielelezo 5.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha tabia za maumbo katika vitenzi alivyopewa na kupata alama 0.

Watahiniwa 85,640 sawa na asilimia 31 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa hao walibainisha kwa usahihi tabia za maumbo ya vitenzi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa majibu sahihi kwa vipengele: (e) **ni**- kitenzi kishirikishi, (f) **-ji**- urejeshi wa mtenda, (g) **vi-** idadi (wingi)**,** (h) **gwa**- kauli ya utendwa**,** (i) **-ika** - kauli ya utendeka, *lakini* alishindwa kubainisha tabia za maumbo ya vitenzi kwa baadhi ya vipengele: (a) **futa**- *kitendo cha kuondoa* badala ya kuamuru, (b) **Hu**- *njeo wakati uliopita*, badala ukanushi, (c) –**tu**- *njeo wakati uliopo wingi* badala ya nafsi ya kwanza wingi, na (d) –hu- *kauli ya kutenda* badala ya hali ya mazoea na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 5.2**


5. (a) Futa mbao
Ni kitenzi kinaonyesha tabia ya wakati (wakati uliopo timilifu)
(b) Hu → Inaonyesha tabia ya ukanushi
(c) Tu → Inaonyesha tabia ya nafsi (nafsi ya tatu umoja)
(d) Hu → inaonyesha tabia ya mazoea tendo linalotendeka mara kwa mara'
(e) Ni → Inaonyesha tabia ya sifa ya kitu.
(f) Ji → Inaonyesha uyakinishi
(g) Vi → huonyesha wingi wa kitu au vitu.
(h) Kigwa → Inaonyesha ~~maana~~ hali ya kutendwa
(i) Ika. → Inaonyesha tabia ya kauli ya kutendeka.

**Kielelezo 5.2:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha tabia za vitenzi zilizokolezwa wino kwa baadhi ya vipengele kama inavyoonekana na kushindwa katika vipengele (a), (c), (e) na (f).

Aidha, asilimia 2.7 sawa na watahiniwa (7,537) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 3.5 hadi 5. Watahiniwa hao waliweza kubainisha kwa usahihi tabia za maumbo katika vitenzi walivyopewa katika vipengele vyote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) aliweza kubainisha umbo **futa** kuwa ni “kuamrisha”, kipengele (b) umbo **hu**-“tabia ya ukanushi”, kipengele (c ) umbo **-tu- “** nafsi ya kwanza wingi”. Pia aliweza kubainisha vizuri tabia za maumbo ya vitenzi katika vipengele (d) - (i) kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 5.3.

**Kielelezo 5.3**



5 a) Kuamrisha
b) Tabia ya ukanushi
c) Nafsi ya kwanza wingi
d) Njeo ya wakati wa mazoea
e) Kitenzi kishirikishi
f) Urejeshi wa mtenda
g) Urejeshi wa mtendwa na kudokeza wingi
h) Tabia ya kutendwa
i) Tabia ya kutendeka

**Kielelezo 5.3**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi na kupata alama zote.

### 2.2.4 Swali la 6: Aina za Maneno na Mjengo wa Tungo

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, mada ndogo ya *Aina za Maneno na Mjengo wa Tungo*. Swali lililenga kupima uundaji na lilikuwa na jumla ya alama (5). Swali lilimtaka mtahiniwa katika kipengele (a) aeleze maana na dhima ya kiunganishi katika sentensi, (b) atunge sentensi mbili kwa kila kiunganishi alichopewa.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 97.5 sawa na watahiniwa (351,325) kati ya wote waliofanya mtihani. Miongoni mwao, asilimia 94.5 sawa na watahiniwa (321,456) walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 6**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 212,850 sawa na asilimia 60.6 walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu 3.5 – 5. Hali hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Aina za Maneno*. Kufaulu vizuri katika swali hili kulitokana na uwezo wao katika kueleza maana ya kiunganishi kuwa ni *neno au kikundi cha maneno chenye kuunganisha maneno, kikundi cha maneno, kishazi au sentensi* na kueleza dhima ya viunganishi kuwa ni *kuunga vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa*. Pia, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutofautisha matumizi mbalimbali ya maneno *kwa sababu, kama, ingawa, lakini* na hivyo kuweza kutumia kama viunganishi na kutunga sentensi kwa usahihi. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza maana na dhima za viunganishi kisha kutunga sentensi kwa kutumia viunganishi hivyo kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**


6. a) Kiunganishi ni aina ya neno ambalo linaunganisha neno na neno au sentensi na sentensi.

Dhima ya kiunganishi katika sentensi ni:-
-kuunganisha sentensi na sentesi ili kutoa maana kamili.

b) i) kwa sababu
-Mama amenipa zawadi kwa sababu nimefaulu vizuri mtihani yangu.
- Amina amechapwa kwa sababu amechelewa.

ii) kama
-Mwalimu amesema kama umefeli utoke mbele.
-Lazima ufaulu kama umesoma kwa bidii.

iii) ingawa
- Juma amefeli ingawa amesoma kwa bidii
-Asha amechelewa ingawa kwao ni karibu.

iv) lakini
- Kwao ni mbali lakini amewahi shuleni
- Soma sana lakini kumbuka kusali.

**Kielelezo 6.1:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutoa maana na dhima ya viunganiski kisha kutunga sentensi kwa kutumia viunganishi kulingana na matakwa ya swali.

Asilimia 33.9 sawa na watahiniwa (108,606) walifaulu kwa kiwango cha wastani. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kutoa maana ya kiunganishi kama ni *aina ya neno au kikundi cha maneno chenye kuunganisha maneno, kirai, kishazi au sentensi* na wengine walishindwa kueleza dhima yake katika kipengele (a). Vivyo hivyo, katika kipengele (b) baadhi ya watahiniwa waliweza kutunga sentensi kwa baadhi ya viunganishi walivyopewa kwa usahihi na kushindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga sentensi kwa kutumia viunganishi (i) *kwa sababu,* alikimbia kwa sababu alikuwa ameiba; Pendo alianguka kwa sababu aliteleza, (ii) *kama,* nitashukuru sana kama utanisaidia kupata viza; angefaulu vizuri kama angesoma kwa bidii. Aidha, mtahiniwa huyo alishindwa kutunga sentensi kwa kutumia kiunganishi (iii) *ingawa* kwa kuandika *ingawa* hakusoma alifaulu; ingawa hakuja tulifurahi, (iv) *lakini* wewe unamjua; *lakini* sisi hatukuwepo; majibu ambayo yalikuwa si sahihi katika kipengele cha (iii) na (iv) na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kipengele (b) kwa kutunga sentensi moja iliyo sahihi badala ya mbili kama ilivyostahili.

**Kielelezo 6.2**


6 a/ Kiunganishi - Ni silabi inayowekwa kati ya sentensi na sentensi ile kuleta maana kamili.
b/ (i) Alienda hospitali kwa sababu alikuwa anaumwa
(ii) Nitakuja kwenu kama wija kwetu
(iii) Alionesha umahiri mkubwa Ingawa alikuwa na umri mdogo
(iv) Ninakupenda lakini haunipendezi.

**Kielelezo 6.2:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga sentensi pungufu na kushindwa kueleza maana na dhima ya kiunganishi katika kipengele (a) na kupata alama za wastani.

Watahiniwa 29,869 sawa na asilimia 5.5 kati ya wote waliojibu swali hili walipata alama za chini 0 hadi 1. Watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutambua aina za maneno na mpangilio wake katika tungo na hivyo kushindwa kueleza maana ya kiunganishi na dhima yake kuwa ni *neno au kikundi cha maneno chenye kuunganisha maneno, kikundi cha maneno, kishazi au sentensi*. Dhima yake ni *kuunga vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa kisarufi kama vile nomino na nomino, kitenzi na kitenzi au kishazi na kishazi.* Pia, watahiniwa hao walishindwa kutunga sentensi kwa

kutumia viunganishi (i) *kwa sababu*, (ii) *kama* (iii) *ingawa* na (iv) *lakini* kutokana kutojua matumizi ya aina za maneno hususani viunganishi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana na dhima ya kiunganishi isiyo sahihi na kutunga sentensi kwa kutumia viunganishi alivyopewa mwanzoni mwa sentensi na hivyo kutofanya kazi ya kiunganishi. Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana na dhima ya kiunganishi na kutunga sentensi zisizozingatia dhima ya kiunganishi na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 6.3**



6 a) Dhima ya kiunganishi katika Sentensi
- Husimama kama kiunganishi cha Jambo au kipereka taarifa

b) i)-kwa Sababu ni mzima ataenda Shule
- kwa Sababu nimefaulu lazima niende lee na masoma

ii)-kama hufanyi mtihani toa taarifa
- kama baba yako mzima tumshukuru Mungu

iii)-Ingawa ninaumwa lazima Shule niende
- Ingawa nimefaulu Lazima nimshukuru mungu

iv)-lakini si wote waovu
- lakini subiri kwanza usichukue uamuzi

**Kielelezo 6.3**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga sentensi kwa kuanza na kiunganishi na hivyo kuharibu dhima ya viunganishi. Pia, alishindwa kueleza maana na dhima ya kiunganishi katika kipengele (a).

### 2.2.5 Swali la 7: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno*. Swali hili lililenga kupima uundaji na lilimtaka mtahiniwa abainishe njia

tatu za kuambatanisha maneno na kisha atoe mifano miwili kwa kila njia aliyoibainisha.

Watahiniwa 258,250 sawa na asilimia 71.7 walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu ambapo watahiniwa 101,590 sawa na asilimia 39.3 walifaulu kwa kiwango cha wastani na cha juu. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa wengi 156,660 sawa na asilimia 60.7 walifaulu kwa kiwango cha chini na kupata alama za chini 0 hadi 1. Miongoni mwao, asilimia 40.8 walipata alama 0 kutokana na kushindwa kubainisha njia hata moja kati ya njia tatu za kuambatanisha maneno kama vile kurudia neno, kuunganisha maneno mawili tofauti hususani N + N au T + N, na kuunganisha maneno mawili huku ukidondosha baadhi ya herufi. Watahiniwa hao pia walishindwa kutoa mifano miwili yenye maneno yanayotokana na uambatanishaji. Kiwango cha chini cha kufaulu kinaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu uundaji wa maneno ya Kiswahili kwa njia ya uambatanishaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja kutokana na kutoelewa matakwa ya swali alitaja baadhi ya vitenzi na kuvinyumbua huku akibainisha dhima ya unyumbuaji huo. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 7.1**


7. i) huweza kutoa maana zaidi ya moja
mfano
i) Piga – Pigana
ii) Imba – Imbana
ii) huweza kutenganisha maana
Mfano
i) Lia – liliwa
ii) Soma - someka
iii) huweza kubadilisha kitenzi kwenda nomino
mfano
i) Maembe yetu
ii) Mtoto analia

**Kielelezo 7.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha dhima ya unyumbuaji badala ya kubainisha njia tatu za kuambatanisha maneno na mifano yake.

Watahiniwa 98,492 sawa na asilimia 38.1 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kubaini baadhi ya njia za uambatanishaji kwa usahihi na kushindwa kutoa mifano dhahiri kwa kila njia. Wengine walichanganya baadhi ya njia za uambatanishaji na kutoa mifano yenye mfanano kwa njia walizobaini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja njia ya kuunganisha maneno na kutoa mfano wa neno "msikwao" linalotokana na uunganishaji wa maneno na udondoshaji wa baadhi ya herufi. Hivyo, mtahiniwa huyo alipungukiwa na hoja na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 3,098 sawa na asilimia 1.2 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango cha juu kwa kupata alama 3.5 hadi 5. Watahiniwa hao walionesha kuelewa matakwa ya swali na pia kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uundaji wa maneno. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa majibu kwa kubainisha njia tatu za kuambatanisha maneno vizuri na kutoa mifano miwili kwa kila njia. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 7.2**



7. (a). Njia ya mwambatano.
Mfano.
i) Mwana + Kwetu → Mwanakwetu.
ii) Askari + Kanzu → Askarikanzu.
(b) Njia ya kuondosha baadhi ya vitamkwa
Mfano.
i) Mkwea + minazi → Mkwezi
ii) Chakula + cha jioni → Chajio
(c). Njia ya kufupisha maneno.
Mfano.
i) Upungufu wa Kinga mwilini → UKIMWI
ii) Baraza la Kiswahili Tanzania → BAKITA.

**Kielelezo 7.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa kutaja njia tatu za kuambatanisha maneno kisha akatoa mifano miwili kwa kila njia.

## 2.3 SEHEMU C: UANDISHI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomhitaji mtahiniwa kuwa na maarifa ya uandishi wa barua rasmi, kirafiki/kindugu na matangazo ya biashara.

### 2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Barua

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Uandishi wa barua* na lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa atofautishe muundo wa barua rasmi na barua ya kirafiki /kindugu na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 42.1 sawa na watahiniwa (151,811) kati ya wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 82.1 sawa na watahiniwa (124,594) walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 10. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 8**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 47.7 sawa na watahiniwa (72,358) waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 kutokana na kukosa maarifa toshelevu kwa baadhi ya vipengele vya muundo katika uandishi wa barua za kirafiki na barua rasmi. Watahiniwa hao walitoa baadhi tu ya hoja za kutofautisha miundo ya barua za kirafiki/kindugu na barua rasmi, ili hali wengine kutokuelezea mazingira ya miundo ya barua hizo. Kwa mfano, katika kipengele cha *salamu*, baadhi yao hawakuonesha namna salamu hizo zinavyotofautiana katika miundo ya barua hizo. Pia, katika kipengele cha *jina na saini ya mwandishi* walishindwa kutofautisha kwa kuonesha kuwa barua ya kirafiki ina jina na saini ya mwandishi badala ya *barua rasmi huwa na saini na jina la mwandishi* ambapo barua ya kirafiki huwa na *jina la mwandishi tu bila saini*. Pia, baadhi ya watahiniwa hawakutoa ufafanuzi wowote kuhusu kipengele cha mwanzo wa barua katika kutofautisha miundo ya barua hizo na hivyo kutotosheleza hoja hiyo ambapo walitakiwa kutofautisha hivi; *mwanzo wa barua ya rasmi huhusu mahusiano ya kikazi* lakini *barua ya kirafiki huhusu undugu wa wahusika kulingana na utamaduni*. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja sahihi kwa kutofautisha baadhi ya vipengele vya muundo wa barua rasmi na kirafiki/kindugu na kushindwa katika vipengele vingine na hivyo kupata alama za wastani.

**Kielelezo 8.1**

8: Barua, Ni Karatasi yenye Ujumbe fulani. Katika barua Kuna aina Kuu mbili za barua nazo ni barua rasmi na barua za Kirafiki/ Kindugu.

Katika Barua Kuna muundo mbalimbali za barua rasmi na barua za Kirafiki/Kindugu nazo ni Kama ifuatayo:-

Anuwani, Katika barua ya Kirafiki Kuna anuwani moja ambayo ni anuwani ya mwandishi, Pia Kwenye barua rasmi Kuna anuwani mbili ambazo ni anuwani ya mwandishi na Anuwani ya mwandiki waji.

Saini, Katika barua ya Kirafiki huwa aihaina Saini ya mwandishi bali huwa na jina la mwandishi, Pia barua rasmi huwa ina Saini pamoja na jina la mwandishi.

Mwanzo wa barua (Kichwa cha barua), Katika barua ya Kirafiki huwa Kuna Salamu na haina Kichwa cha barua, Pia barua rasmi huwa Kuna Salamu pamoja na Kichwa cha barua.

Tarehe, Katika barua ya Kirafiki huwa inaKuwa na hotarehe, Pia barua rasmi huwa haina tarehe inakuw na Kumbukumbu namba Kama imetolewa.

Pamoja na hayo muundo wa barua rasmi na barua za Kirafiki inaweza iKamchanganya mtu yule ambaye hajui Kuandika barua hizo, hivyo basi inapaswa uwe na muundo moja Katika barua.

**Kielelezo 8.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetofautisha muundo ya barua rasmi na barua ya kirafiki/kindugu kwa kutozingatia kipengele cha tarehe na kutoa maoni ya kupinga miundo ya barua hizo katika hoja ya mwisho.

Asilimia 34.4 sawa na watahiniwa (52,236) walifaulu vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kutofautisha kwa usahihi muundo wa barua rasmi na barua za kindugu/kirafiki kwa kuzingatia *idadi ya anwani, kumbukumbu namba, kichwa cha habari/barua, salamu, saini na jina la mwandishi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa toshelevu kuhusu miundo ya barua rasmi na kirafiki/kindugu kwa kutoa hoja zenye ufafanuzi wa kina katika kutofautisha miundo ya barua hizo. Aidha, walielezea mazingira ya miundo hiyo kwa kila aina ya barua kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitofautisha kipengele cha anwani kwa kuandika, barua rasmi

huwa na anwani mbili ambapo anwani ya mwandishi *hukaa juu kulia* na anwani ya mwandikiwa *hukaa kushoto mwa karatasi* lakini barua ya kirafiki/kindugu ina anwani moja ambayo ni ya mwandishi tu. Hata hivyo, mtahiniwa huyo aliendelea kuonesha tofauti za kimuundo katika vipengele vingine vya barua hizo na kupata alama za juu. Kielelezo 8.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyefafanua vipengele vinavyotofautisha miundo ya barua za kikazi/rasmi na kirafiki/kindugu kwa usahihi.

**Kielelezo 8.2**


8 (b). TOFAUTI KATI YA BARUA RASMI NA YA KIRAFIKI

Barua ni maandishi yanayoandikwa katika karatasi maalumu ili kupitisha ujumbe kuhusu kuomba kazi au kutuma salamu. Kuna aina mbili za barua barua rasmi na barua ya kirafiki zifuatazo ni tofauti kati ya barua hizo.

Barua rasmi huwa na ~~anw an~~ anuani mbili ambayo ni anuani ya mwandishi na anuani ya mwandikiwa ambayo hukaa ~~kulia~~ kushoto mwa karatasi lakini barua ya kirafiki ina anwani moja ambayo ni ya mwandishi.

Barua rasmi huwa na kichwa cha habari ambacho huandikwa kwa kifupi katikati ya karatasi kwa maandishi makubwa na kupigiwa mstari. Lakini barua ya kirafiki haina kichwa cha habari.

Barua rasmi huwa na sahihi na jina la mwandishi ambapo huanza sahihi alafu jina linafuata lakini barua ya kirafiki huwa na jina peke yake bila ya sahihi.

Barua rasmi mwishoni lazima iwe na cheo cha ~~mwa~~ mwandishi lakini barua ya kirafiki huwa haina cheo mwishoni.

Barua rasmi huwa na kumbukumbu namba ambayo huandikwa kushoto upande wa anuani ya mwandikiwa lakini barua ya kirafiki haina kumbukumbu namba.

Barua rasmi hutakiwa kuwa fupi na kutumia lugha fasaha bila ya kutumia lugha ya mtaani! Lakini barua ya kirafiki huweza kuandikwa hata kwa kutumia lugha ya mtaani.

**Kielelezo 8.2:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri kwa kutofautisha muundo wa barua rasmi na barua za kindugu/kirafiki.

Aidha, watahiniwa 27,217 sawa na asilimia 17.9 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5 kutokana na kushindwa kutofautisha muundo wa barua rasmi na barua za kirafiki/kindugu. Baadhi ya watahiniwa walionesha kutoelewa matakwa ya swali hilo kwa kuandika kadi za mialiko, barua za wahariri na wengine waliandika matangazo ya kazi na biashara mbalimbali kinyume na maelekezo ya swali. Aidha, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu miundo ya barua mbalimbali na hivyo kushindwa kutofautisha muundo wa barua rasmi na barua ya kirafiki/kindugu ambapo walitakiwa kutoa hoja kama vile: *Barua rasmi ina anwani zaidi ya moja tofauti na barua ya kirafiki huwa na anwani moja; barua rasmi huwa na kichwa cha habari tofauti na barua ya kirafiki isiyo na kichwa cha habari; barua rasmi huwa na jina na saini ya mwandishi tofauti na barua ya kirafiki yenye jina pekee*. Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha muundo wa barua rasmi na barua za kindugu /kirafiki kwa kuandika barua ya kirafiki iliyo katika muundo wa kadi ya mwaliko kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 8.3**


BARUA YA KIRAFIKI

08.

Napenda kuku alika wewe rafiki yangu
mpendwa kwenye happy barday yangu
itakayo fanyika tarehe 1-12-2018
ukumbi wa nluzu . pia unaombwa
usikose kuta kuwa na madiko diko ya
kutosha . Napenda kuwa karibisha wote
Nd, Jamaa, Marafiki, Ml n.k
EMMANUEL PAUL
Unaombwa usikose .

BARUA YA KINDUGU

Napena kuwakaribisha Nd, Jm, Ml, Ps
kwenye sherehe yangu ya kuzaliwa
Mimi BONIFAS PAUL
Napenda kuwakaribishani nyote ni
nayo furaha kubwa sana kuwaka
ribisha, Itakayo fanyika ukumbi wa
ngodejo kuanzia saa 8:00 mchana
mpaka saa 12:00 jioni unaombwa
kufika bila kukosa .

**Kielelezo 8.3**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha muundo wa barua rasmi na barua za kirafiki /kindugu.

### 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Matangazo

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Uandishi wa Matangazo* na lililenga kupima maarifa. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika tangazo kuhusu biashara ya mchele na jina lake liwe Pera Mlavi na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 202,730 sawa na asilimia 56.3 kati ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Miongoni mwao, asilimia 95 sawa na watahiniwa (192,562) walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani na kulifanya kuwa swali lililojibiwa vizuri zaidi na idadi kubwa ya watahiniwa. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 9**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 63.9 sawa na watahiniwa (129,458) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa kuandika tangazo ambalo halikuzingatia baadhi ya vigezo vya uandishi wa tangazo. Baadhi ya watahiniwa waliandika tangazo bila kuandika kichwa cha tangazo ambapo walitakiwa *kuandika* 'BIDHAA SAFI YA MCHELE'. Wengine hawakuzingatia maelekezo ya kutumia jina la mtoa tangazo yaani *Pera Mlavi* badala yake waliandika majina yao binafsi. Vile vile, baadhi hawakuweka mawasiliano ya mtoa tangazo kama vile *anwani* au *namba ya simu* na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika tangazo

lisilojitosheleza kwa baadhi ya vigezo muhimu vya kuzingatiwa katika uandishi wa tangazo.

**Kielelezo 9.1**


9

TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

Jipatie mchele safi na salama kutoka kwa Bwana Pera Mlavi. Mchele huu na mzuri kutoka mbeya na unaiva vizuri kabisa. Mchele unapatikana kwa bei ya jumla na reja reja. Duka letu lipo Kariakoo mtaa wa Michikichi pembeni kidogo ya benki ya NMB

Nyote mnakaribishwa

Kwa Mawasiliano zaidi, Piga namba.

0745711696

"Mchele Safi Kwa wote"

**Kielelezo 9.1**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuandika tangazo bila kuzingatia *kichwa cha tangazo, sanifu* na *jina la mtoa tangazo* na kupata alama za wastani.

Asilimia 31.1 sawa na watahiniwa (63,104) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uandishi wa matangazo. Watahiniwa hao waliweza kuandika tangazo kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo, kutumia lugha sanifu na matumizi sahihi ya alama za uandishi. Taratibu muhimu za uandishi wa tangazo ni pamoja na kutumia maneno machache, herufi kubwa na kuzingatia kichwa cha tangazo, "*BIDHAA SAFI YA MCHELE*", sababu za tangazo, sifa za kitu/bidhaa inayotangazwa "*bidhaa safi daraja la kwanza*", maelezo zaidi kuhusu biashara/jambo linalotangazwa kama vile, "*ubora wa bidhaa ,vifungashio imara na ujazo*" na mawasiliano ( jina, anwani/simu/ *barua pepe*) ya mtoa tangazo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuandika tangazo la uuzaji wa mchele kutoka Kyela kwa kuzingatia taratibu zote na kupata alama za juu kama kielelezo Na. 9.2 kinavyoonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 9.2**

9.

TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

VUNJA BEI NA MCHELE WA KYELA

MCHELE SAFI UNAUZWA NDANI NA NJE YA
NCHI. NI MCHELE SAFI KUTOKA KYELA NA UMETAYARI-
SWA KWA KUTUMIA MASHINE ZA KISASA KABISA.
BEI ZETU NI KARIBU NA BURE. FIKA SASA KARIAKOO
MTAA WA MSIMBAZI AU KWA MAWASILIANO PIGA
SIMU NAMBA 0784171462 PERA MLAVI

WAHI SASA KWANI WATEJA 10 WA MWANZO WATAPE
WA PUNGUZO LA ASILIMIA 15 YA BEI
MTEJA KWETU NI MFALME.

**Kielelezo 9.2**: Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa aliyeandika kwa usahihi tangazo kwa kuzingatia vigezo muhimu licha ya kuwa na tatizo dogo la kitahajia katika neno 'umetayariswa' badala ya u*metayarishwa*.

Watahiniwa 10,168 sawa na asilimia 5 pekee ndio waliojibu swali hili na kufaulu kwa kiwango cha chini cha alama 0 hadi 2.5. Watahiniwa hao waliandika tangazo lisilokidhi taratibu nyingi za uandishi wa tangazo. Baadhi ya watahiniwa walionesha hali ya kukosa maarifa kuhusu uandishi wa tangazo kwa kuzingatia vigezo muhimu; wengine kutokuelewa matakwa ya swali hilo na hivyo kuandika matangazo yasiyohusiana na mada ya "biashara ya mchele". Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika tangazo lililohusu "Nafasi za Kidato cha Tano kwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne", kutokana na kushindwa kuzingatia kichwa/mada ya tangazo alilopewa, na mwingine aliandika tangazo linalohusu “BIASHARA YA VIPODOZI” badala ya “*BIASHARA SAFI YA MCHELE*”, kama kielelezo Na. 9.3 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa wa aina hii.

**Kielelezo 9.3**




**Kielelezo 9.3**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika tangazo la biashara ya vipodozi kinyume na matakwa ya swali na kupata alama hafifu.

## 2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lililomhitaji mtahiniwa kuwa na maarifa kuhusu kukua na kuenea kwa Kiswahili kabla ya uhuru.

### 2.4.1 Swali la 10: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili enzi za Waarabu*. Swali lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa kueleza sababu nne (4) zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 317,207 sawa na asilimia 88 ya waliofanya mtihani. Miongoni mwao watahiniwa 235,741 sawa na asilimia 74.3 walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 10. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 143,078 sawa na asilimia 45.1 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6. Watahiniwa hao walitoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja katika kueleza sababu nne zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni. Baadhi ya watahiniwa walieleza kwa usahihi baadhi ya sababu hizo kama vile:

> *Lugha ya Kiarabu kutumika kutolea mafundisho ya dini ya kiislam, biashara ya utumwa na pembe za ndovu iliyoendeshwa kwa lugha mseto kati waarabu na wenyeji na hivyo kiasi kikubwa cha msamiati wa kiarabu kusanifishwa na mwingiliano wa waarabu na wenyeji kutokana na kuoana na hivyo msamiati wa Kiarabu kuingizwa kwa kiasi kikubwa katika lugha ya Kiswahili*.

Watahiniwa wengine walitoa sababu zingine zisizo sahihi kama vile, *asili ya lugha ya Kiswahili ni Kiarabu* na pia *waarabu walikipenda sana Kiswahili* hoja ambazo hazina uhalisia wowote miongoni mwa sababu zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa sababu zisizojitosheleza kuhusu sababu za Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 10.1**



10. Lugha ni sauti za nasibu zenye maana na kutumika katika jamii kwa mawasiliano.

Sababu zinazofanya lugha ya kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu ni kutokana na;

Dini, waarabu walianzisha dini katika nchi ya Tanzania na za kiafrika na maneno ya dini hiyo yakazoeleka katika lugha ya kiswahili na kuongezeka katika lugha ya kiswahili.

Elimu, katika suala la elimu waarabu walipokuja nchini walianzisha elimu yao ya kislamu na nyenginezo ambazo zilichangia ongezeko la maneno ya kiarabu katika lugha ya kiswahili.

Utawala, Waarabu walipokuja nchini na kututawala walikuwa wanatumia lugha ya kiarabu nchini Afrika na waafrika baadhi yao walitumia lugha hiyo baada ya kuondoka kwa waarabu waafrika na hapa nchini tulikuwa kichwani tunabaadhi ya maneno ya kiarabu na hiyo basi kuweza kuchanganya na lugha ya kiswahili na kusababisha lugha ya kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu.

Kutokutawaliwa na baadhi ya nchi, Afrika kutawaliwa na waarabu kwa kipindi kirefu na nakutokutawaliwa na nchi zengine na kutookongezeka kwa maneno ya nchi zingine toka na nchi ya kiarabu. Na hiyo basi hizo ndizo sababu zilizofanya kuongezeka kwa maneno katika lugha ya kiswahili.

**Kielelezo 10.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa sababu zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni bila kutumia mifano ya maneno ya kiarabu yaliyopo katika lugha ya Kiswahili.

Asilimia 29.2 sawa na watahiniwa (92,663) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kutoa hoja nyingi sahihi kuhusu sababu zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni. Majibu ya watahiniwa hao kwa jumla yalionesha uelewa mkubwa wa watahiniwa kuhusu sababu za kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za waarabu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa sababu kama vile; *shughuli za kibiashara, ndoa, utawala* na *dini* na kupata alama za juu kama kielelezo Na. 10.2 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 10.2**


10. Lugha ni mpangilio wa Sauti za nasib
u uliyokubalika katika jamii kama njia
ya mawasiliano. Zifuatazo ni Sabab
u za zilizofanya kiswahili kuwa na man
eno mengi ya lugha ya kiarabu.
Utawala, Miongoni mwa Sababu-
Zilizopelekea Kiswahili kuwa na maneno
o mengi ya kiarabu ni utawala waarabu w
alitawala pwani mwa afrika mashariki na
kupelekea lugha yao kuwa na maneno amba
ya yanaendana na kiswahili Mfano, neno
wakili kwa kiarabu ni Wakil au neno kal
amu ni Qalam.
Shughuli za biashara, Miongoni mwa
Sababu zilizopelekea kiswahili kuwa na
maneno mengi ya lugha ya kiarabu ni bia
shara waarabu walijihusisha na biashara ka
tika pwani za afrika mashariki na kupele
kea lugha yao kuathiri lugha ya kiswahi
li.
Ndoa, Baadhi ya waarabu wengi wali
okuja katika pwani za afrika mashariki
walioweza kufunga ndoa na wazawa na ku
pelekea kuunda hati za ndoa ambazo pia
zilisababisha na kupelekea lugha ya kisw
ahili kuwa na misamiati au maneno meng
i ya lugha ya kiarabu kuliko lugha nyingi
ne.
Dini, Sababu zilizopelekea lugha ya
kiswahili kuwa na misamiati mingi ya lug
ha ya kiarabu ni dini kwa Sababu waarabu
walijitahidi sana kusambaza dini ya kiislam

**Kilelezo 10.2** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa sababu nne za lugha ya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu kuliko lugha zingine za kigeni.

Aidha, asilimia 25.7 sawa na watahiniwa (81,466) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5 kutokana na kushindwa kujibu swali hili vizuri. Baadhi ya watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kubainisha njia mbalimbali za uundaji wa misamiati kama vile “Njia ya miambatano”, “Urudufishaji” na “kutohoa maneno” na wengine, walitoa sababu za Sultan Sayyed Said kuhamishia makazi yake Zanzibar ili kuimarisha utawala wake, majibu ambayo si sahihi, badala ya kueleza sababu nne zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya kiarabu kuliko lugha zingine za kigeni kama vile:

> *waarabu kuwa watawala wa mwanzo katika pwani ya Afrika Mashariki na hivyo msamiati wake kufahamika zaidi*, *lugha ya Kiarabu kutumika kutolea mafundisho ya dini ya kiislam*, *ujirani*

*uliopo baina ya nchi za kiarabu na pwani ya Afrika Mashariki, biashara ya utumwa na pembe za ndovu iliyoendeshwa kwa lugha mseto kati waarabu na wenyeji na hivyo kiasi kikubwa cha msamiati wa kiarabu kusanifishwa na mwingiliano wa waarabu na wenyeji kutokana na kuoana na hivyo msamiati wa Kiarabu kuingizwa kwa kiasi kikubwa katika lugha ya Kiswahili na kusanifishwa.*

Kielelezo 10.3 kinathibitisha majibu ya mtahiniwa huyo aliyejibu swali hili kwa kutokuelewa matakwa ya swali na kupata alama 0.

**Kielelezo 10.3**

10. Lugha ni sauti zanasibu zenye kuleta
maana iliyokubaliwa katika jamii fulani
Zifuatazo ni sababu zilizokifanya
Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu
kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni
njia ya mwambatano: hapa maneno
mawili huunganishwa kukuleta maana
kamili mfano mwana + hewa – mwanahewa
mwana + jeshi – mwanajeshi – mwana + nchi
mwananchi hii ni sababu mojawapo zilizo
kifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi
ya Kiarabu
Urudufishaji: ni kitendo cha kurudia
mika maneno kwakurudia rudia mfano.
Polepole, sawasawa, vilevile na Barabara hii
ni mojawapo ya sababu zilizokifanya Kiswa
hili kuwa na maneno mengi ya kiarabu
kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni
Kitendo cha kupachika: hii ni
kitendo cha kupachika viambajengo kab
la na baada ya mzizi wa neno mfano
lima - lim - mcheze - chez

10. Kutohoa maneno: ni kitendo cha
kuchukua baadhi ya maneno au irupi na
kuunda neno jipya hii ni mojawapo ya sababu
zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno
mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nying
ine za kigeni
hivyo basi lugha ni sauti za nasibu
zenye kuleta maana zilizokubaliwa katika
jamii fulani.

**Kielelezo 10.3**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa kuandika njia za uundaji wa maneno badala ya kueleza sababu zilizokifanya Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni.

## 2.5 SEHEMU E: FASIHI KWA UJUMLA

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano yaliyomtaka mtahiniwa kuwa na maarifa, uwezo wa kuchambua, kutathmini na kuunda ili kutoa maana na matumizi ya methali, kuhakiki vitabu teule vya fasihi andishi pamoja na kutunga utenzi.

### 2.5.1 Swali la 11: Uhakiki wa Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Methali*. Swali lililenga kupima maarifa na lilimtaka mtahiniwa kueleza maana na matumizi ya methali zifuatazo: (a) Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu jua (b) Mchimba kisima huingia mwenyewe, (c) Ukiona zinduna ambari iko nyuma, (d) Waarabu wa Pemba wanajuana kwa vilemba na (e) Mbaazi ukikosa maua husingizia jua. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache (36,494) sawa na asilimia 10.1 pekee ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa cha chini ambapo watahiniwa 6,460 sawa na asilimia 17.7 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 11**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 30,034 sawa na asilimia 82.3 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama za chini 0 hadi 4. Miongoni mwao, asilimia 37.4 sawa na watahiniwa (13,667) walipata alama 0 kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa methali ambapo watahiniwa hao walishindwa kueleza maana

na matumizi ya methali (a) hadi (e) kwa kutoa majibu tofauti na yale yaliyotarajiwa. Baadhi ya watahiniwa walitoa maana na matumizi ya methali tofauti na zile walizopewa kama ambavyo mtahiniwa mmoja alitoa maana na matumizi ya methali isemayo, "Mwenda pole hajikwai", methali isiyokuwepo katika swali hili. Wengine waliandika methali zinazokaribiana kimaana na methali walizopewa kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa ufafanuzi wa methali "Mbaazi ukikosa maua husingizia jua" kwa kuandika 'Ukiona vyaelea vimeundwa'. Majibu ya watahiniwa hao na mengine mengi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali.

Katika kujibu swali hili, mtahiniwa alitakiwa kufafanua maana na matumizi ya methali kama ifuatavyo: Katika kipengele (a) *Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu jua* humaanisha kupata kingi kwa mara moja ni bora zaidi kuliko kidogo kidogo kwa siku nyingi, hutumika kuwashauri watu kujaribu kupata mahitaji kulingana na haja kwa wingi; (b) *Mchimba kisima huingia mwenyewe* humaanisha aanzishaye ubaya humrudia mwenyewe, hutumika kuwaonya watu wenye tabia ya kuwakomoa wengine ili wasije wakajikuta wanaathirika wenyewe; (c) *Ukiona zinduna ambari iko nyuma* humaanisha kutukia kwa jambo moja husababisha kutokea kwa jambo jingine, hutumika kuonesha vitu au matendo yanayotokea kwa pamoja na huwashauri watu kuwa makini kwa tukio moja linapotokea; (d) *Waarabu wa Pemba wanajuana kwa vilemba* humaanisha watu wenye mienendo au tabia za aina moja hujuana wenyewe na hufanana kwa matendo yao, hutumika kupumbaza hadhira ili kufanikisha lengo kwa wahusika; na (e) *Mbaazi ukikosa maua husingizia jua* humaanisha mtu akishindwa jambo hutoa visingizio vingi, hata kama mwenyewe ndiye sababu ya kushindwa, hutumika kuelezea tabia za watu katika jamii kutoa visingizio kila wanaposhindwa kufanikisha jambo fulani. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana na matumizi katika methali zote alizopewa.

**Kielelezo 11.1**


11 Kueleza maana ya methali zifuatazo.

(a) Kivuli cha mimbo hakimfichi mtu jua.

- Kivuli cha babu hakuwanji chawa.

(b) Mchimba kisima huingia mwenyewe.

- Mwenda pole hajikwai.

(c) Ukiona zinduna ambari iko nyuma.

Ukiona vya elea ujue vimeundwa.

(d) Waarabu wa pemba wanajuana kwa vilemba.

Waarabu wa pemba wanajuana kwa vilemba.

(e) Mbaazi ukikosa maua husingizia jua.

Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.

**Kielelezo 11.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana na matumizi ya methali kwa kutaja methali zilizo kinyume na methali husika na kunakili baadhi ya methali kinyume na matakwa ya swali.

Watahiniwa 5,488 sawa na asilimia 15 walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 kutokana na kueleza maana na matumizi ya methali kwa usahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kipengele (b), (d), na (e) kwa usahihi kwa kutoa majibu yafuatayo: (b) a*anzishaye jambo baya huweza kumrudia mwenyewe,* ikitumika kuonya watu wanaoanzisha mambo kwa nia mbaya wajue yanaweza kuwarudi, *(d) watu wenye tabia zinazofanana hujuana kwa mienendo yao wenyewe,* hutumika kueleza tabia za watu wanaofanana na (e) *ashindwaye jambo hutoa visingizio vingi*, ikitumika kuelezea tabia za watu katika jamii wanaotoa visingizio kila wanaposhindwa kufanikisha jambo fulani.

Aidha, mtahiniwa huyo alishindwa kutoa maana na matumizi katika kipengele (a) ambapo aliandika, 'Kidogo kidogo hujaza kibaba' na katika (c) aliandika 'Maji yakimwagika hayazoleki' majibu ambayo yanaonesha hali ya kupinga methali alizopewa badala ya kueleza maana na matumizi yake. Mtahiniwa huyo alitakiwa kueleza katika (a) *kupata kingi kwa mara*

*moja ni bora kuliko kodogo kidogo kwa muda mrefu ikitumika kushauri watu kupata kingi kwa mara moja ni bora kuliko kidogokidogo;* na katika (c) *ukiona jambo moja linatokea ujue lingine linafuata ikitumika kuonya watu wanapoona jambo limetokea wachukuwe tahadhari kwani jambo jingine linafuata*.

Watahiniwa 972 sawa na asilimia 2.7 pekee ndio waliojibu vizuri swali hili kwa kueleza maana na matumizi ya methali walizopewa na kufaulu kwa kiwango cha juu kuanzia alama 10 hadi 15. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi maana na matumizi ya methali nne (4) hadi tano (5) walizopewa katika kipengele, (a) hadi (e). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote na kupata alama zote kama sampuli ya majibu ya mtahiniwa huyo yanavyoonekana katika kielelezo Na. 11.3.

**Kielelezo 11.3**

11 (a) sehemu yenye kipato kidogo hakiwezi kumudu mahitaji kwa wote.
Methali hii inatoa matumizi kwamba kitu kidogo hakiwastiri wengi
(b) Mtu anayejitaftia matatizo hujitia mwenyewe
- Methali inatoa matumizi kwamba kila anayejitafutia matatizo mwisho wake huishia pabaya.
(c) ukiona dalili mbaya ujue kuna kitu kinafuata.
ukiona isha mbaya ujue kuna jambo linakuja kutokea.
(d) Watu wenye ustaarabu wanajuana kwa busara zao
watu waliostaarabika huweza kujuana wenyewe.
(e) Mtu asipoweza kutimiza malengo husingizia amelogwa
Methali hii inatukumbusha kuwa uvumilivu tuweze kuwa
(e) wenye kuvumilia pale tunapokosa jambo na sio kuwa
watu wenye kulalamika

**Kielelezo 11.3:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa kueleza maana na matumizi ya methali alizopewa kwa usahihi na kupata alama za juu.

### 2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Ushairi)* na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha ukweli wa kauli kuwa, "washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili" kwa kutoa hoja kutoka katika diwani mbili teule. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache 146,569 sawa na asilimia 40.7 kati ya wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Swali lilijibiwa vizuri na watahiniwa wengi (137,544) sawa na asilimia 93.8 walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 12**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 61 sawa na watahiniwa (89,399) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 10 hadi 15 kwa kuweza kuthibitisha ukweli wa kauli kuwa '*Washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayowakabili*' kwa kutoa hoja tatu sahihi kwa kila diwani kutoka diwani mbili walizosoma. Watahiniwa hao waliweza kuthibitisha kwa kuandika hoja mbalimbali zilizokidhi haja ya swali kama vile, kutoa utangulizi mzuri uliokuwa unafafanua maneno 'kuelimisha jamii' kuwa ni *kitendo cha kuipa elimu jamii kwa nia ya kuiasa au kuionya juu ya jambo fulani*. Katika kiini waliweza kutumia diwani mbili kati ya tatu walizosoma katika kuthibitisha ukweli wa kauli hiyo kwa kuwa walikuwa wamezisoma na kuelewa maudhui yake ipasavyo.

Kwa mfano, katika diwani ya "*Malenga Wapya"* walitoa hoja kama vile, *msanii anaelimisha jamii kwa kutokumnyanyasa mwanamke, kuwa na mapenzi ya kweli na kupiga vita matabaka*. Vivyo hivyo katika diwani ya "*Wasakatonge*" walieleza namna msanii anavyoelimisha jamii yake kuhusu; *viongozi kuacha tabia ya kung'ang'ania madaraka, athari za kutegemea misaada na jamii ipambane dhidi ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana.* Vilevile, katika diwani ya "Mashairi ya Chekacheka" msanii anaelimisha jamii kuhusu *ulaghai wa viongozi walio madarakani, washairi kuwa wazi na kuonesha maovu yanayojitokeza katika jamii* na *wapendanao kujitoa kwa dhati kwa ajili ya wale wawapendao*.

Pamoja na kutoa hoja hizo, watahiniwa hao waliweza kunukuu baadhi ya mistari katika beti za mashairi mbalimbali ili kuthibitisha ukweli wa kauli kuwa "Washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili." Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia shairi la 'Madikteta' katika diwani ya "Wasakatonge" kuelezea namna uongozi mbaya unaweza kuleta migogoro katika jamii. Pia katika diwani ya "Malenga wapya" ameeleza suala la mapenzi ya dhati huleta amani na upendo katika jamii, kwa kutumia shairi la 'Ua'. Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 12.1**

12. Kuelimisha jamii ni kitendo cha kutoa elimu katika wanajamii ili kuweza kufanya mambo yao kikufasaha. kwakutumia mashairi mawili niliyo yasoma tunaona jinsi yalivyo elimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili jamii ~~nikianza na~~ diwani hizo ni WASAKATONGE iliyo andikwa na M.S. khatibu pamoja na MALENGA WAPYA iliyo andikwa na TAKILUKI. Ni kianza na shairi La Wasakatonge. tunaona kuna elimu iliyo ikabili jamii hiyo.

Ugombezi wa madalaka; ni kitendo cha kugombea ajila moja kwa watu wawili au zaidi ya hao. Mshairi ameonasha dhamira hii katika shairi La tonge La ugali huku akionesha jinsi viongozi wanavyo gombaniana madaraka kwa ugomvi

"Wakitukanana, wakigombana kwa tonge la ugali"

Hivyo basi tunaona katika jamii watu waki wa wana gombaniana madaraka

Ufisadi; ni kitendo cha kuhujumu ma hali za mtu kwa kutumia maneno ya ulaghai Mwandishi ameonesha dhamira hii katika shairi La miamba ~~wa~~ jinsi watu waliyo kuwa wanafisadi wenzao

"Hivyo nyote ni vyakwangu"

tunaona katika jamii watu wakiwa wana ~~fisadi~~ hujumu mali za wenzao kwa ulaghai

Uwongozi mbaya; ni kitendo cha kuongoza vibaya nchi au jamii yako kwa


Mila za Kigeni Uchochea Mmomonyoko wa maadili Katika jamii. Mfano wa Shairi ambalo huonesha Ukweli huu ni "Jiwe simchi" Katika jamii wanaiga tabia Ya Kusagana Kwani hii si tabia Nzuri na Inaweza Kupelekea mmomonyoko wa maadili. Kupitia hali hii watu wanapata Elimu dhidi ya mambo haya na watu wanapata Kuelimika.

Kwa Kutumia Diwani nyingine ya "MALENGA WA PYA" Kilicho andikwa na TAKILUKI ametoa Elimu nyingi Katika jamii Kama zifuatazo.

Utumiaji wa Sukari Kupwingi Unaweza Kuleta madhara ya Ugonjwa wa Kisukari, Mfano wa Shairi ni "Matumizi Ya Sukari" Shairi hili Limeeleza dhidi ya madhara ya Sukari mwilini. Kupitia hali hii au Elimu hii watu wanajua Kumbe Kuna athari Kubwa Kwa Kutumia Sukari Kupwingi.

Mapenzi ya dhati Uleta amani na Upendo Katika jamii. Mfano wa shairi ni Shairi la "Ua" shairi hili limeonesha Mapenzi ya dhati baina ya watu Katika jamii. Hapa watu wamepata elimu ya Kuwa Mapenzi ya dhati Uleta amani na Upendo Katika jamii Kwahiyo yatupasa tuzingatie.

Kuwepo Kwa Unyonyaji Katika jamii Kunaweza Kupelekea dhuruma na Uonevu Kwa watu Katika jamii. Mfano wa Shairi la "SAMAKI MTUNGONI" Mshairi ameonesha Kuwepo Kwa Unyonyaji Katika jamii na hii aifai Katika jamii. Kupitia haya watu Katika jamii wanapata Elimu Kubwa Kuhusiana na Unyonyaji wa watu Katika jamii Kuna madhara makubwa.

**Kielelezo 12.1**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyethibitisha kwa usahihi ukweli wa kauli kuwa washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili.

Watahiniwa 48,145 sawa na asilimia 32.8 walifaulu swali hili kwa kupata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuthibitisha kauli kuwa, "Washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili". Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja sahihi lakini walishindwa kuzitolea mifano kutoka katika diwani husika ili kuthibitisha maelezo hayo, pia wengine katika utangulizi na hitimisho hawakuweza kufafanua vizuri kauli waliyopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi usioendana na matakwa ya swali kwa kuandika kuwa, *si kweli washairi hutumia mashairi katika kuelimisha jamii bali hutumia dhamira/ujumbe pekee*. Utangulizi huo ulimpunguzia mtahiniwa huyo alama japokuwa alitoa hoja sahihi katika

kiini. Watahiniwa wengine walishindwa kufafanua kwa usahihi hoja walizotoa na hivyo kutotosheleza matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alithibitisha kauli kwa kutoa hoja katika diwani ya “Mashairi ya cheka cheka” kuhusu ulaghai wa viongozi waliopo madarakani lakini hakuifafanua hoja yake kwa kutumia mfano sahihi wa shairi badala yake akatumia shairi la ‘Hatuna kauli’ lililopo katika diwani ya "Wasakatonge" hivyo kukosa alama katika hoja hiyo na kupata alama za wastani. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa hoja zisizojitosheleza.

**Kielelezo 12.2**



12. Washairi ni watu wanaotunga mashairi. Kwa kutumia mashairi mawili ambayo ni "wasakatonge" na "Malenga wapya" nitathibitisha kauli isemayo "washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili"

Kwa kuanza na "wasakatonge" iliyoandikwa na M.S.Khatibu nitathibitisha ukweli wa kauli hii:

Katika shairi la "wasakatonge" msanii ametuonyesha jinsi watu wanavyofanya kazi kwa bidii lakini bado wanapata kipato kidogo ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji yao.

Katika shairi la "Jiwe simchi" mshairi anatuonyesha jinsi watu wanavyofanya vitendo vya ajabu kwa kusagana watu wenye jinsia moja.

pia katika shairi la "matabaka" mshairi anatuonyesha kuwa kuna tabaka la maskini yaani watu wasiojiweza na tabaka la matajiri watu wenye uwezo.

pia tukiangalia katika shairi la "Malenga wapya" iliyoandikwa na TAKILUKI nitathibitisha.

Uongozi mbaya, katika shairi la "puuzo" tunaona jinsi watu wanavyonyanyaswa na viongozi wao na wakati wamechagua wenyewe na viongozi walitoa kampeni nyingi wakati wauchaguzi lakini hawatekelezi.

Katika shairi la "Kwanini?" tunaona jinsi wanaume kuwa wanavyowatoroka wake zao usiku na kuwaacha peke yao.

**Kielelezo 12.2:** Sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutaja mashairi na kuyaelezea bila kuthibitisha jinsi mashairi hayo yanavyoelimisha jamii.

Licha ya kuwa na kiwango cha juu cha kufaulu katika swali hili, asilimia 6.2 sawa na watahiniwa (9,025) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama za chini 0 hadi 4. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha

katika kuthibitisha kauli kuwa “Washairi hutumia mashairi yao kuelimisha jamii kuhusu mambo yanayoikabili.” Baadhi ya watahiniwa walionesha kutokuelewa matakwa ya swali hili na kujibu kinyume na matarajio ya swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua dhamira mbalimbali katika diwani za "Wasakatonge" na "Malenga Wapya" bila kuonesha jinsi washairi wanavyoelimisha jamii kwa kutumia mashairi yaliyopo katika diwani husika. Katika diwani ya “ *Wasakatonge*” alitoa hoja ya *ugombezi wa madaraka* kuwa ni kitendo cha kugombea ajira moja watu wawili huku akitumia shairi la 'Tonge la ugali', bila kuelezea *athari za kugombea madaraka kunavyorudisha nyuma juhudi za maendeleo ya jamii.* Vile vile, katika diwani ya "Malenga Wapya" mtahiniwa alielezea dhamira ya 'unyonyaji' kama ni kitendo cha kuwanyonya watu wa hali ya chini kwa kutumia nguvu huku akitumia shairi la 'bahari'**,** bila kuonesha namna gani mshairi anaelimisha jamii kupinga unyonyaji. Kielelezo 12.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja mashairi na kubainisha dhamira kwa baadhi ya mashairi hayo kutoka diwani ya "Wasakatonge" na "Malenga Wapya" bila kuzitolea maelezo yoyote namna msanii alivyoelimisha jamii na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 12.3**


1SHAIRI ISRAFU
DHAMIRA MATUMIZI MABAYA YA MAL
Mfano: Kumbuka kuna kujuta,
Nawe mja wa kupata...
Shairi Punzo
Dhamira SWALA LA MATABAKA
Mfano: Ofisini ukifika, Pitika wanajitia,
Haja unayoitaka, Mwenyewe tajifanyia
Na katika diwani nyingine ya WAS
AKATONGE tunaona washairi wanavyo
elimisha jamii kwa mfano katika ma
shairi yetu yafuatayo.
Shairi WASAKATONGE
Dhamira Swala la matabaka.
Mfano: Na wabeba dege wamaroshani,
Ni msukuma mkokoteni...
Shairi UA
Dhamira SWALA LA UDIKTETA
Mfano Twajua huamwa Afrika,
sana inatitika...
Shairi TOHARA
Dhamira MATATIZO YAKE
Mfano: Tohara kwa wanawake.

**Kielelezo 12.3**: Sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeataja mashairi bila ufafanuzi wowote kuhusu washairi wanavyoelimisha kwa kutumia mashairi yao na kupata alama za chini.

### 2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya.

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Riwaya*) na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha hoja kuwa "mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila" kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu katika riwaya mbili teule. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 257,574 sawa na asilimia 71.4 kati ya wote waliofanya mtihani huu. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo watahiniwa 218,417 sawa na asilimia 84.8 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 13 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 13**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Miongoni mwao, watahiniwa 131,052 sawa na asilimia 50.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 4.5 hadi 9.5 kutokana na kuthibitisha hoja kuwa "mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila" kwa kutoa baadhi ya hoja zikiwa sahihi na zingine kuzitolea maelezo yasiyojitosheleza. Katika kujibu swali hilo, baadhi ya watahiniwa walichanganya wahusika kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kutumia wahusika wa riwaya ya "Watoto wa mama N'tilie" alimtumia mhusika Dotto kama mtoto wa kike badala ya *Kurwa*. Aidha, watahiniwa wengine walitaja majukumu mbalimbali ya wahusika wa kike katika riwaya hizo badala ya kueleza huruma na fadhila aliyonayo mwanamke inavyomfanya atende majukumu aliyonayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" na kuelezea jinsi Mama ntilie

alivyoamua kumlea Kurwa kwa sababu alimuona ni mtoto wa mtaani badala ya kuonesha *huruma na fadhila za Mama N'tilie zilizosababisha kumlea Kurwa ingawa si mwanae wa kumzaa*. Pia, katika riwaya ya "Takadini" mtahiniwa anatoa hoja kwa kueleza mapenzi ya dhati aliyonayo Shingai kwa Takadini badala ya kueleza *huruma na fadhila aliyokuwa nayo Shingai iliyomfanya kumpenda Takadini kwa dhati.* Kielelezo 13.1 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuthibitisha hoja kuwa "mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila"

**Kielelezo 13.1**

13 Mwanamke ni mtu mwenye jinsia ya
kike ambaye ni mmoja kati ya watu Muhimu
Sana katika malezi ya familia. Ni kweli
mwanamke ni mtu mwenye huruma na
fadhira nyingi katika familia kwa kutumia
riwaya Mbili nilizosoma ambazo ni :-
"TAKADINI" na "WATOTO WA MAMA N'TILIE"
zifuatazo ni fadhira na huruma zilizofanywa
na Mwanamke kwakuanza na riwaya ya
Takadini iliyoandikwa na Ben. J. Hanson (MBJ)
mwanamke amechorwa kama ifuatavyo;
Mwenye Mapenzi ya dhati, katika jamii
yoyote wapo watu wenye mapenzi kwa wazazi
wao, ndugu zao, nchi zao na hata wapenzi
wao. Hata katika ~~...~~ riwaya ya Takadini
mwandishi amemchora mhusika Shinghai amba
ye alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Takadini
ingawa alikuwa sope na pia mhusika Sekai
alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Mwanaye
Takadini aliyekuwa sope.
Mwana mapinduzi. Katika jamii wapo
baadhi ya wanawake ambao ni wasomi na wenye
msimamo na hivyo huwapelekea kubadili jamii,
Hata katika riwaya ya Takadini mwandishi
amemchora Mhusika Shinghai ambaye ali
weza kuipindua jamii yake kwa kuwa na
mpenzi sope (Takadini) na kupata mtoto ambaye
sio sope hivyo alielimisha jamii juu la
swala la ubaguzi wa rangi.

**Kielelezo 13.1**: Sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kurudia hoja na kutotosheleza matakwa ya swali.

Watahiniwa wengine 87,365 sawa na asilimia 33.9 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 10 hadi 15 kwa kuwa waliweza kuthibitisha hoja kuwa, “mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila” kwa kuonesha namna mwanamke alivyokuwa na huruma na fadhila katika kutekeleza majukumu yake. Watahiniwa hao walitumia vitabu teule viwili vya riwaya huku wakiwatumia wahusika sahihi katika riwaya hizo katika kuthibitisha hoja juu ya huruma na fadhila za mwanamke. Kwa mfano, katika riwaya ya “Takadini” watahiniwa waliweza kuwaelezea wahusika kama Sekai, Pindai, Shingai na Ambuya ambao walikuwa na moyo wa huruma na fadhila. Mhusika *Sekai* alitoroka na mwanae ili kumnusuru kifo kwa kuwa alikuwa sope, *Pindai* (kumtetea Sekai kwa wake wenza), *Shingai* (kukubali kuolewa na Takadini japo ni sope) na *Ambuya* (kumtetea mtoto sope asiuawe). Pia katika riwaya ya “Watoto wa mama N’tilie” wahusika kama Mama Ntilie, Zenabu na Kurwa ambapo *Mama N’tilie (*kulea watoto wake pamoja na magumu yote*), Zenabu* (kulea watoto wa Mama N'tilie) *na Kurwa* (kumtetea Peter asipigwe na Dotto). Hivyo hivyo katika riwaya ya "Joka la Mdimu" wahusika kama mke wa Brown Kwacha, mke wa Tino na Katibu wa Brown Kwacha wameoneshwa kuwa ni wanawake wenye huruma na fadhila katika jamii yao iliyokuwa na uonevu na isiyojali maslahi ya wengi. Kielelezo 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja toshelevu kwa kutumia riwaya ya “Watoto wa mama N’tilie” na “Takadini” na kuzifafanua vizuri kulingana na matakwa ya swali.

**Kielelezo 13.2**

13. Mwanamke ni mtu muhimu sana katika jamii. Lakini mwanamke huyo pia ndiye anayedharauliwa. Hata hivyo kwenye riwaya ya Takadini iliyoandikwa na Ben Hanson pamoja na riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo mwanamke ameonekana kama mtu mwenye huruma na fadhila. Kwa kutumia wahusika Sekai, Tendai na Pindai katika riwaya ya ~~H~~ Takadini wamechorwa kama watu wenye huruma na fadhila;

Sekai. Huyu ni mhusika mkuu. Ni mama wa Takadini na ni mke wa Mzee Makwati. Sekai aliishi bila ya kupata mtoto kwa muda wa miaka tisa hivyo baada ya kupata mtoto mwenye ulemavu wa ngozi (sope), aliambiwa na wazee wa kijiji kuwa inabidi mwanawe auawe. Hivyo sekai alikataa kwa kuwa alikuwa na huruma pamoja na uchungu juu ya mwanawe.

Pindai. Huyu ni mke mwenza wa Sekai. Mzee Makwati alikuwa na wake wanne ambao ni Pindai, Sekai, Dadirai na Rumbidzai. Dadirai na Rumbidzai walikuwa wakimtusi na kumfanyia fitina Sekai lakini Pindai aliweza kuwa upande wa sekai siku zote na kumtetea juu ya jambo lolote. Hivyo Pindai alikuwa ni mtu mwenye huruma sana pamoja na fadhila.

Tendai, ~~Baada ya Sekai~~ Huyu alikuwa ni rafiki wa sekai. Baada ya Sekai kukimbia kijijini kwao kwa nia ya kumuokoa mwanawe alifika katika kijiji kingine ambapo hakuwa na rafiki yeyote isipokuwa Tendai. Tendai aliweza kumshauri Sekai pale alipokuwa na tatizo na aliweza kumsaidia. Hivyo hata Tendai naye ni mtu mwenye huruma.

13. Katika riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie wahusika kama Mama n'tilie, Zenabu na Kurwa wamechorwa kama watu wenye huruma na fadhila,

Mama n'tilie, Huyu ni mhusika mkuu. Ni mama wa Peter na Zita na ni mke wa Mzee Lomolomo. Huyu ni mwanamke ambaye alihangaika sana ili kupata hela itakayoweza kukidhi hoja ya nyumbani kwake pamoja na kuwanunulia watoto wake sare za shule na pia kuwalipia ada ya shule. Na pia ni mwanamke mwenye huruma na fadhila kwani aliweza kumlea Kurwa kama mtoto wake aliyemzaa.

Zenabu, Huyu ni Jirani wa Mama n'tilie. Zenabu aliishi na familia ya mama n'tilie kama ndugu zao. Aliweza kumsaidia Peter chakula pale alipokosa chakula. Na pia alimsaidia Zita alipoumwa kwa kukodi teksi iliyompeleka Zita hadi hospitali. Aliwajali na kuwalea watoto wa Mama n'tilie pale ambapo hakuwepo. Hivyo Zenabu ni mtu mwenye huruma na fadhila.

Kurwa, Ni msichana aliyesaidiwa na Peter. Kurwa alikuwa ni mtoto yatima ambaye hakuwa na wazazi aliishi na ndugu yake ambaye alifariki. Hata hivyo Kurwa alikuwa na huruma kwani aliweza kumsaidia Peter pale alipopigwa na nduguye Doto. Pia alimsaidia kutafuta chakula hapo jaani. Hivyo hii inaonyesha kwamba Kurwa alikuwa ni mtu mwenye huruma.

Pia katika riwaya zetu kuna wanawake ambao hawana huruma katika riwaya ya Takadini kuna Badirai, Rumbidzai na Chiodo pia katika riwaya ya Watoto wa Mama n'tilie kuna Zita.

**Kielelezo 13.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyethibitisha hoja kuwa mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila kwa usahihi na kupata alama za juu.

Watahiniwa 39,157 sawa na asilimia 15.2 walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama za chini 0 hadi 4 kwa kuwa walitoa majibu yasiyo sahihi katika hoja nyingi. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kutoa utangulizi ili kuthibitisha hoja kuwa, mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila ambapo wengine walikanusha hoja hiyo kinyume na matakwa

ya swali. Pia wapo waliojadili dhamira mbalimbali zilizopo katika riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua dhamira ya ulevi katika riwaya ya “Watoto wa Mama N’tilie” akielezea suala alilokuwa nalo mzee Lomolomo na katika riwaya ya "Takadini" alieleza, imani za kishirikina katika jamii, masuala ambayo si sahihi katika kuthibitisha huruma na fadhila ya wanawake katika riwaya hizo.

Watahiniwa hao walitakiwa kuthibitisha hoja hiyo katika riwaya teule kama ifuatavyo: Katika riwaya ya “Takadini” wahusika kama Sekai (alimhurumia mwanae asiuawe), Pindai (alimtetea Sekai kwa wake wenza dhidi ya kuawa yeye na mwanae), Shingai (alikubali kuolewa na Takadini ambaye ni sope) na Ambuya (alimtetea mtoto sope asiuawe). Pia katika riwaya ya “Watoto wa mama N’tilie” wahusika kama Mama Ntilie (alilea watoto wake, Kurwa na mumewe bila kujali aliyokuwa anatendewa na mumewe), *Zenabu* (alilea watoto wa Mama N'tilie alipokuwa hayupo) *na Kurwa* (alimtetea Peter asipigwe na Dotto). Hivyo hivyo katika riwaya ya "Joka la Mdimu" wahusika kama mke wa Brown Kwacha, mke wa Tino na Katibu wa Brown Kwacha wameoneshwa kuwa ni wanawake wenye huruma na fadhila katika jamii yao iliyokuwa na uonevu na iliyowanyanyasa wanawake. Kielelezo 13.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za chini kwa kutoa hoja chache katika kuthibitisha kuwa mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila.

**Kielelezo 13.3**

13. Mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila". Thibitisha hoja hiyo kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kutoka kati ka vitabu viwili vya riwaya kati ya vilivyoorodheshwa.

Kwa kutumia riwaya mbili nilizosoma nitaelezea jinsi mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila na nitaanzia na WATOTO WA MAMAN'TILIE mwandishi wake E. MBOGO (H.P) pamoja na JOKA LA MDIMU mwandishi ni A. J. SAFARI (H.P).

Nikianza na kitabu cha WATOTO WA MAMAN'TILIE mwandishi E. MBOGO. Katika kitabu hiki kinaonesha kuwa mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhila kama pale ambapo maman'tilie alikuwa na huruma na watoto wa na mme wake alikuwa akirudi amelewa na kumpiga mke wake. Pia mama n'tile alikuwa ni mtu mwenye fadhila sana katika jamii yake inayomzunguka. Pia maman'tile alikuwa ni mwanamke mpambanaji sana kuhusu watoto wake.

Pia nilikiangalia kitabu kingine nilichosoma ambayo ni JOKA LA MDIMU, mwandishi wake ni A. J. SAFARI inaonesha kuwa mwanamke alikuwa mpambanaji na mwenye fadhila kwa wenzake wanaomzunguka. Pia mzee lumulumo alikuwa akimuonea sana mke wake lakini mwanamke aliendelea kuvumilia na kuwa na huruma na fadhila kwa mme wake huyu.

Nikimalizia kwa kusema kuwa katika hivi vitabu vya riwaya nilivyosoma vilikuwa vina mwelezea mwanamke vizuri juu ya tabia yao ilivyokuwa kama maman'tile alivyokuwa mpambanaji na mpenya bi ahara aliye makini sana katika mambo yake.

**Kielelezo 13.3:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa isiyo na utangulizi na yenye hoja moja kwa kila kitabu kutoka riwaya Mama N'tilie na Joka la Mdimu kinyume na matakwa ya swali.

## 2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi (Uhakiki wa Tamthiliya*) na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa akanushe kauli kuwa waandishi wa tamthiliya wameshindwa kufikisha ujumbe kwa jamii

iliyokusudiwa kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili teule alizosoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 249,854 sawa na asilimia 69.3 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo asilimia 89.9 sawa na watahiniwa (224,554) walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 14 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 14**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 60.9 sawa na watahiniwa (152,211) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 10 hadi 15. Watahiniwa hao waliweza kukanusha kauli kuwa waandishi wa tamthiliya wameshindwa kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa kwa kutoa hoja tatu kwa kila tamthiliya kati ya tamthiliya mbili teule. Katika kukanusha kauli hiyo, watahiniwa walionesha namna waandishi wa tamthiliya walivyoweza kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa, kwanza; walitoa utangulizi mzuri na unaoendana na matakwa ya swali kwa kukanusha kauli hiyo kuwa, *waandishi wa tamthiliya hawajashindwa kufikisha ujumbe kwa jamii waliyoikusudia bali wameweka wazi yale yote yaliyopo katika jamii walizoziandikia*. Pili; wametumia tamthiliya teule na kuonesha jumbe mbalimbali zilizokusudiwa na waandishi katika tamthiliya hizo kama vile, "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe"; ujumbe unaotolewa kwa jamii ni kuhusu *uzembe, uvivu, ulevi na ukosefu wa elimu*. Katika tamthiliya ya "Orodha"; ujumbe unaofikishwa kwa jamii ni pamoja na tahadhari ya ugonjwa hatari wa UKIMWI unaosababishwa na *ulevi, ukosefu wa elimu, tamaa/starehe, ukosefu wa uadilifu na kukosa uaminifu katika ndoa.* Pia

katika Tamthiliya ya "Kilio Chetu" mwandishi anatoa ujumbe kuhusu *Ugonjwa wa UKIMWI usivyo na tiba, Wazazi kutoa elimu ya jinsia kwa watoto wao* na *starehe iliyopitiliza ni chanzo cha ugonjwa hatari wa UKIMWI*. Tatu; watahiniwa hao walitoa hitimisho zuri lililofafanua vyema umuhimu wa tamthiliya hizo kwa jamii. Kielelezo 14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea kwa usahihi namna waandishi walivyofikisha ujumbe kwa jamii.

**Kielelezo 14.1**

14. Serikali inapaswa kushughulikia suala la huduma duni za kijamii: Kutokana na uwepo wa huduma duni za kijamii kama vile huduma ya afya na elimu na maji, serikali inapaswa kushughulika ipasavyo kwa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Katika tamthiliya, watoto hawaendi shule kwani shule ziko mbali, na huduma ya afya ni duni kwani hospitali ziko mbali:

"... Shule i mbali ..."

Imani za kishirikina hukwamisha ~~im~~ maendeleo ya jamii: Imani za kishirikina ni imani potofu zinazozuia maendeleo ya jamii nzima. Katika tamthiliya hii, uhesabuji wa watu katika kijiji cha Balozi Mitomingi unakwama kwani wananchi wengine wanaamini kuwa wachawi tu ndio wanaohesabu watu ili wawaroge.

"Kama ututuhesabu basi wewe u mchawi..."

Zifuatazo ni hoja tatu kutoka katika tamthiliya ya KILIO CHETU ya Medical Aid Foundation:

Ugonjwa wa UKIMWI hauna tiba: UKIMWI ni kifupi cha Ukosefu wa Kinga Mwilini. Ugonjwa huu husababishwa na Virusi vya UKIMWI (VVU). Ugonjwa hauna tiba, ila una kinga. Katika tamthiliya hii, Joti ni mwathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Yeye ameathirika kwa kupitia ngono zembe na wanawake kadhaa. Mjomba anaishauri na kuwapa elimu familia ya Joti juu ya ugonjwa huo. Mjomba anapingana na Jirani ambaye aliwashauri wazazi wa ~~j~~ Joti kumpeleka kwa mganga wa jadi "mtaalamu":

"... tunatakiwa tumpeleke kwa mtaalam..."

Wazazi wanapaswa kutoa elimu ya kijinsia kwa watoto wao: Wazazi wanajukumu la kuwapa watoto wao elimu ya kijinsia ili watoto hao waweze kuepukana na ngono zembe na mapenzi katika umri mdogo kwani watakuwa wanajua adha za kufanya hivyo. Katika tamthiliya hii, Mama

14. Suzi na Baba Joti wamekataa kuvunja ukimya huku wakibaki na msimamo wao wa kuwaadabisha watoto wao na fimbo. Hii ni kinyume na mtazamo wa Baba ~~Joti~~ Anna na Mjomba ambao wanasisitiza wazazi kuvunja ukimya na kuongea na watoto wao. Hawa wanapingwa na Mama Suzi:

"... hicho ndio nini, kaka? Huko si kunifundishia mwanangu umalaya...."

Mapenzi katika umri mdogo ni hatari: Mapenzi katika umri mdogo ni hatarishi kwani watoto hawajapevuka vyema kisaikolojia na ~~kib~~ kimwili, hivyo kuwasababishia matatizo mbalimbali, yakiwemo magonjwa ya ngono kama vile UKIMWI, kisonono, na mimba za utotoni. Hii ni dhahiri kupitia Joti ambaye alipata UKIMWI na Suzi aliyepata mimba katika umri mdogo. Hii inathibitika pale Suzi anapomwambia Anna:

Suzi: "... nina mimba ...."

Hivyo, waandishi wa tamthiliya wameweza na wamefaulu katika kufikisha ujumbe kwa jamii / hadhira iliyokusudiwa. Medical Aid Foundation na Bwana Semzaba wameweza kuelimisha jamii kupitia kipengele cha maudhui cha ujumbe kwa wanajamii hususani vijana.

**Kielelezo 14.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekanusha kwa usahihi kauli kwa kutoa hoja madhubuti kutoka katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" na "Kilio Chetu".

Watahiniwa wengine 72,343 sawa na asilimia 29 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama za 4.5 hadi 9.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja. Baadhi ya watahiniwa hao hawakuweza kuandika utangulizi mzuri wenye kufafanua kauli hiyo kulingana na matakwa ya swali. Pia, watahiniwa wengine walitoa hoja kwa kutaja dhamira zilizopo katika tamthiliya teule bila kuonesha ujumbe unaotokana na dhamira hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea suala la ulevi lilivyokuwa katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" badala ya kuonesha ujumbe wa mwandishi katika suala hili ambapo *ulevi kurudisha nyuma maendeleo ya jamii.* Aidha, wapo watahiniwa waliokanusha kauli waliyopewa kwa usahihi lakini wakashindwa kutoa hoja zenye mifano madhubuti kutoka katika riwaya teule na

kupata alama za wastani. Kielelezo 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyethibitisha kauli kwa kutoa hoja bila kufafanua kwa mifano madhubuti kutoka tamthiliya teule na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 14.2**

14 Ujumbe ni maneno yanayo tolewa na mwandishi
wa kazi za fasihi ili kuleta maana
Mwandishi amefikisha ujumbe kwa jamii
Katika tamthilia ya kilio cheo.
Imani potofu mwandishi amefikisha ujumbe kwa
kupitia pale ambapo mama suzi alikambia na
jirani yake mama anna kuwa binti yake suzi
Kakuwa na amfundishe elimu ya kujitambua
mama suzi na kukataa nakusema mtoto wake
mdogo hawezi kumwambia mambo makubwa
Kamahayo Hatimae suzi alipata ukimwi na
mimba.
Ngono ambapo joti huwachukua picha zake
Kina mwalami na kuwapeleka kwenye mbanda
ya picha za ngono na yeye kuwa na mahusiano
na muuza vitumbua hatimae kupata ukimwi na
Kufa.
Tamaa ambapo suzi alikuwa na tamaa na
Kununuliwa chipsi na joti na kwenda nae kufanya
mapenzi na kupata mimba pia na hata ukim
wi.
Katika kitabu cha ngoswe penzi kitovu cha
uzembe ambapo mwandishi kafikisha ujumbe
kwa hulewa zaidi
Imani potofu ambapo mama wa kwanza
kukataa kuesabiwa na kumwambia ngoswe
kuwa nyinyi si nyonya damu kwa sababu
walikuwa hawana elimu kuhusu uwandishi

**Kielelzo 14.2**: Sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja kwa kuelezea matukio kutoka katika tamthiliya teule bila kutoa mfano wowote unaobainisha ujumbe wa mwandishi.

Watahiniwa 25,300 sawa na asilimia 10.1 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 4. Watahiniwa hao walishindwa kukanusha kauli

kuwa “Waandishi wa tamthiliya wameshindwa kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa". Baadhi ya watahiniwa katika utangulizi walikubali kauli kwamba waandishi wa tamthiliya wameshindwa kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa badala ya kukanusha kauli hiyo kwa kuonesha namna waandishi wa tamthiliya walivyoweza kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Pia watahiniwa walitakiwa kutumia tamthiliya teule na kuonesha jumbe mbalimbali zilizokusudiwa na waandishi kama vile; "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe"; ujumbe unaotolewa kwa jamii ni kuhusu *uzembe, uvivu, ulevi na ukosefu wa elimu*. Katika tamthiliya ya "Orodha"; ujumbe unaofikishwa kwa jamii ni pamoja na tahadhari ya ugonjwa hatari wa UKIMWI unaosababishwa na *ulevi, ukosefu wa elimu, tamaa/starehe na ukosefu wa uadilifu na uaminifu katika ndoa.* Pia katika Tamthiliya ya “Kilio Chetu” mwandishi anatoa ujumbe kuhusu *Ugonjwa wa UKIMWI usivyo na tiba, Wazazi kutotoa elimu ya jinsia kwa watoto wao* na *starehe iliyopitiliza ni chanzo cha uonjwa hatari wa UKIMWI*.

Kutokana na kukosa uwezo wa kuchambua maudhui katika tamthilia hizo ili kubainisha jumbe mbalimbali, baadhi ya watahiniwa walielezea maswala mtambuka yaliyopo katika jamii zetu kama vile *ubakaji, mauaji ya albino na vikongwe, wizi wa kutumia silaha na matumizi ya madawa ya kulevya* badala ya kuchambua ujumbe unaopatikana katika tamthiliya alizopewa na wengine walionesha kukubali kauli kuwa waandishi wa tamthiliya wameshindwa kufikisha ujumbe kwa jamii wanazoziandikia kama kielelezo Na. 14.3 kinavyonesha jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 14.3**

14. Waandishi wengi wa kazi za fasihi hasa tamthilia wamekuwa wakiandika na kuandaa kazi zao na kushindwa kufikisha ujumbe kwa jamii inayohusika hivyo wanakuwa wamefeli na kusababisha watu wa jamii hiyo iliyokusudiwa kukosa mwelekeo wa kubadilisha mienendo yao.

Nitakanusha kauli hii kwa kutumia tamthilia mbili nazo ni tamthilia ya Orodha iliyoandikwa na St Steve Reynolds pamoja na tamthilia ya Ngoma ya Penzi Kitovu cha Uzembe iliyoandikwa na Edwin Semzaba.

Kwakuanza na tamthilia ya Orodha tunaona kwamba mwandishi wa tamthilia hii amefeli kuyalenga baadhi ya mambo katika jamii iliyokusudiwa kama vile;

Mwandishi amefeli kuonyesha madhara ya kutokuwa mwaminifu katika ndoa. Katika tamthilia hii tunaona kwamba baadhi ya watu, Mfano Bwana Eko amekosa kuwa mwaminifu kwa Mke wake hivyo ameweza kutoka nje ya ndoa na kutembea na wasichana wadogo kama vile Furaha na Mary na hivyo kujisababishia kupata magonjwa kama vile UKIMWI (Ukosefu wa kinga mwilini)

Mwandishi amefeli kuonyesha njia bora za kujikinga na magonjwa ya zinaa; Mwandishi ameshindwa kutoa njia bora na sahihi ambazo zingeweza kupunguza mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI hivyo kupelekea ugonjwa huo kuenea kwa kasi. Mfano Salim, mchumba yake Furaha aliweza kumuamini mchumba yake hivyo hakuweza kutumia kinga wakati wa kujamiiana naye na hivyo aliweza


14 kuupata ugonjwa huo kwa sababu hata Furaha ali-
kuwa tayari ni muathirika.
Mwandishi ameshindwa kuelimisha jamii kuhusu
elimu ya jinsia; Mwandishi ameshindwa kuunda wah
usika ambao wangekuwa ni washauri vika hivyo ha
wahusika wamekuwa wakifanya ~~matendo~~ Land
oa bila kujali umri na muda wa kufanya vitend
o hivyo na hivyo kusababisha kupata magonjwa. Kw
a Mfano Furaha pamoja na kuwa amehitimu d
arasa la saba lakini hakupewa elimu ya jinsia hivy
o alijikuta kufanya mapenzi kabla ya wakati wake
na hivyo kuambukizwa UKIMWI.
Kwa kuendelea na tamthilia ya Ngoswe Penzi
Kitovu cha Uzembe tunaona kwamba pia mwand
ishi alishindwa kufichua baadhi ya ujumbe kwe
nda sehemu au katika jamii iliyokusudiwa kama
vile;
Mwandishi alishindwa kuwajenga wahusika wake
kutoa malezi bora ya watoto; Wahusika wa tamthilia
hii wamekuwa wakiwachunga watoto wao hasa wa
kike pale wanapofikia umri wa kuolewa na kuw
anyima uhuru wa kuchagua mtu bora na anayew
afaa katika maisha yao ya ndoa. Mfano Mazoea
hakupewa nafasi ya kumchagua mwanaume sahih
i na bora katika maisha yake.
Mwandishi ameshindwa kuonyesha taratibu zina
zotakiwa kufuatwa wakati binti anatakiwa kuolewa
Mwandishi amefeli kuwaonesha uhusika wahusika wa
ke wa kufuata taratibu zote za ndoa pale mtoto w
a kike anaolewa. Mfano Balozi Ngongoa mkeni Mitomio

**Kielelezo 14.2**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kinyume na matakwa ya swali.

### 2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji wa Kazi za Fasihi*, mada ndogo ya *Utungaji wa Ushairi*. Swali lililenga kupima uundaji na lilimtaka mtahiniwa atunge utenzi wenye beti nne (4) juu ya UMUHIMU WA KATIBA MPYA TANZANIA.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 360,392 sawa na asilimia 100 kwa kuwa lilikuwa swali la lazima. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo watahiniwa 211,551 sawa na asilimia 58.7 walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 15 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Jedwali Na. 14:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 41.3 sawa na watahiniwa (148,841) walifaulu kwa kiwango cha chini kwa kupata alama hafifu 0 hadi 4 kutokana na kukosa maarifa mahsusi kuhusu utunzi wa utenzi. Miongoni mwao, watahiniwa 75,231 sawa na asilimia 20.9 walipata 0 kutokana na kushindwa kutunga utenzi kuhusu "Umuhimu wa Katiba Mpya Tanzania." Kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali, baadhi ya watahiniwa walitunga utenzi kuhusu masuala mbalimbali kama vile "*Uhuru wa Tanzania, Rais wetu, Bunge la Tanzania, Shule yetu* na nyinginezo badala ya kutunga utenzi unaoendana na maelekezo ya swali alilopewa ambayo ni 'Umuhimu wa Katiba Mpya Tanzania; Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga utenzi uliohusu *maendeleo, elimu bure, umasikini* na *hospitali kuboreshwa* ambapo ubeti mmojawapo katika utenzi wake unasema,

"Naungana na rais,

Kupongeza lake wazo,
hospital zimeboreshwa,
huduma zote twapata"

Kwa ujumla, utenzi huo haukuzingatia kanuni zozote za utunzi kama vile *urari wa vina na mizani*. Pia, ubeti huo na nyingine alizotunga zilikuwa na maudhui tofauti na usiozingatia matumizi ya lugha sanifu kwa kuandika neno 'hospital' badala ya kuandika *hospitali*. Wengine waliandika nathari/maelezo mafupi kuhusu "*UMUHIMU WA KATIBA MPYA TANZANIA*" kinyume na matakwa ya swali na hivyo kupata alama 0. Kielelezo 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetunga utenzi unaozungumzia masuala tofauti tofauti kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 15.1**

15 Nchi yetu ya sasa,
maendeleo yasonga mbele,
kila kitu fasta fasta,
miundo mbinu twapata,

wazee kwa vijana wanazingatia,
maendeleo ya sasa akunda alie waza,
elimu bure kwa sana,
maskini na tajiri,

Naungana na rais,
kupongeza lake wazo,
hospital zaboreshwa,
Huduma zote twapapata.

15 katika hili nakili,
Umaskini twaliwaga,
Maisha bora kwa sasa,
Ajira zipo wazi,

**Kielelezo 15.1**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutunga utenzi kuhusu "UMUHIMU WA KATIBA MPYA TANZANIA" kwa kutunga utenzi wenye mambo mseto na usio na kichwa cha utenzi.

Asilimia 35 sawa na watahiniwa (126,248) walifaulu kwa kiwango cha juu kwa kupata alama 10 hadi 15. Watahiniwa hao waliweza kutunga utenzi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za utunzi wa utenzi kama vile kichwa cha utenzi kilichoandikwa kwa herufi kubwa, urari wa vina na mizani, utoshelevu, kutumia lugha sanifu na ya kiushairi na kutumia alama za uandishi kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutunga utenzi mzuri kwa kuandika kichwa cha utenzi "*UMUHIMU WA KATIBA MPYA TANZANIA*" kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote za utunzi wa utenzi kama vile, mfanano wa vina vya mwisho vya ubeti na kuzingatia maudhui ya utenzi na kupata alama za juu. Kielelezo 15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetunga utenzi uliojitosheleza kwa kuzingatia kanuni za utunzi wa utenzi.

**Kielelezo 15.2**

15. UMUHIMU WA KATIBA MPYA TANZANIA.

01. Leo nashika kalamu,
Ninalo jambo muhimu,
Katiba mpya muhimu,
Ndugu ninawaambia.

02. Ndugu nawausia,
Nchi imeendelea,
Nyingine zake sheria,
Zimepitwa na wakati.

03. Katiba hii ya sasa,
Muda wake imekosa,
Ili kuepusha visa,
Katiba mpya muhimu.

04. Uchumi wa viwanda,
Tumehitajika panda,
Uchumi wa kati kwenda,
Katiba irekebishwe.

**Kielelezo 15.2**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa kuzingatia taratibu zote za utunzi wa tenzi na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 23.7 sawa na watahiniwa (85,303) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza. Baadhi ya watahiniwa hao walitunga utenzi kwa kuandika kichwa cha utenzi kwa herufi ndogo na wengine hawakuzingatia taratibu za utunzi wa utenzi kikamilifu kama vile urari wa vina na mizani, utoshelevu, kutumia lugha sanifu na ya kiushairi na kutumia alama za uandishi na hivyo kupata alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga utenzi kwa kuandika kichwa cha utenzi kwa herufi ndogo na kutotumia lugha ya kishairi na yenye mvuto kama vile *inkisari, na mazida* ili kuwa na vina na mvuto wa utenzi na hivyo kupata alama za wastani kama kielelezo Na. 15.3 kinavyoonesha.

**Kielelezo 15.3**

| | |
|---|---|
| 15 | Chakutumaini sina, |
| | Ila katiba ya Tanzania, |
| | Jamuhuri iliyotupatia, |
| | katiba mpya Tanzania. |
| | |
| | Miongozo imeandikwa, |
| | Na sheria kutamkiha, |
| | Kila raia imemuhusisha, |
| | katiba mpya Tanzania |
| | |
| | katiba imeandikwa |
| | kwa wote watanzania |
| | Hakuna makukwepeka |
| | katiba mpya Tanzania |

**Kielelezo 15.3**: Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetunga utenzi usiojitosheleza katika idadi ya beti, vina, mizani na usio na kichwa cha utenzi kama ilivyotakiwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA

Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali kumi na tano (15) yaliyotoka katika mada za *Ufahamu na Ufupisho, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Matumizi ya Sarufi, Uandishi, Maendeleo ya Kiswahili, Uhakiki wa Kazi za Fasihi* na *Utungaji wa Kazi za Fasihi*.

Uchambuzi wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa watahiniwa walifaulu katika mada nne kwa kiwango kizuri, mada mbili kwa kiwango cha wastani na mada moja pekee ndio iliyokuwa na kiwango hafifu katika mada zilizotahiniwa. Kiwango kizuri cha kufaulu kilikuwa katika mada zifuatazo; *Uhakiki wa* kazi za *Fasihi Andishi* (89.5%), *Uandishi* (88.6%), *Ufahamu* (74.3%) na *Maendeleo ya Kiswahili* (74.3%).

*Mada ya Matumizi ya Sarufi* (64.1%) na *Kutunga Kazi za Fasihi* (58.7%) zilikuwa na viwango vya wastani vya kufaulu. Aidha, mada ya *Fasihi Simulizi* (17.7%) ilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani huu.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 021 Kiswahili kwa mwaka 2018 kupitia mada mbalimbali kilikuwa kizuri. Wastani wa kufaulu kwa mada zote ni (66.7%). Kiwango hiki kimeshuka kwa asilimia 3 ikilinganishwa na kiwango cha juu cha kufaulu kwa mada kwa mwaka 2017. Hali hii inadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa mwaka 2018.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, Mtihani wa Kidato cha Nne katika somo la Kiswahili mwaka 2018 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani *maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini*. Kiwango cha kufaulu kwa jumla ni kizuri ambapo watahiniwa 320,041 sawa na asilimia 89.32 walifaulu somo hili.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile kutofuatwa kwa maelekezo ya swali na uelewa mdogo wa mada mbalimbali hasa mada za *Fasihi Simulizi, Sarufi*, na *Kutunga kazi za Fasihi*. Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika mtihani wa Kidato cha Nne, mikakati mbalimbali inahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwawezesha

wanafunzi kupata ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha ikizingatiwa kuwa *sarufi* na *fasihi* ndiyo msingi wa taaluma katika ujifunzaji wa lugha.

Kiwango hiki cha kufaulu kinaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji kutiliwa mkazo katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuboresha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa hususani kwa mada zilizoshuka viwango vya kufaulu kwa mwaka 2018 vinapolinganishwa na viwango vizuri vya mwaka 2017. Kwa mfano, mada ya *Kutunga kazi za Kifasihi* imeshuka kwa asilimia 11.8 kutoka kiwango kizuri (70.5%) na kuwa kiwango cha wastani (58.7%) na mada ya *Ufaham*u imeshuka kwa asilimia 12.9 kutoka (87.2%) na kuwa (74.3%). Aidha, mada iliyokuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu ni *Fasihi Simulizi* iliyoshuka kwa asilimia 67.8 kutoka kiwango kizuri (85.5%) na kuwa kiwango hafifu (17.7%).

Mada ya *Fasihi Simulizi* huweza kuboreshwa kwa kutumia mbinu shirikishi na kutoa mazoezi ya kutosha hususani katika kubainisha maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazotumiwa na wanajamii kwa ujumla. Kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia, kipaumbele cha matumizi ya methali kiwekwe katika uwasilishaji wa kazi mbalimbali za kifasihi kama vile masimulizi ya hadithi, vichekesho, maigizo (tamthiliya), maghani, ngonjera na michezo ya watoto (katuni). Aidha, methali zitumike kama sehemu ya utamaduni katika kuadilisha na kuadabisha jamii.

Pia, kumekuwepo na kupanda kwa viwango vya kufaulu vya mada kwa mwaka 2018 kutoka viwango vya kufaulu kwa mwaka 2017. Mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi* imepanda kwa asilimia 7.4 *kutoka* (82.1%) na kuwa (89.5%), *Uandishi* imepanda kwa asilimia 3.4 kutoka (85.2%) na kuwa (88.6%), *Maendeleo ya Kiswahili* imepanda kwa asilimia 39.8 kutoka kiwango cha wastani (34.5%) na kuwa kiwango kizuri (74.3%) na *Matumizi ya Sarufi* imepanda kwa asilimia 16 kutoka (48.1%) na kuwa (64.1%).

Mwisho taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Kiswahili na kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kufaulu kwa viwango vya chini kwa baadhi ya mada ili kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuinua kiwango cha kufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu waweke msisitizo wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya Fasihi simulizi, katika utanzu wa semi, hasa kipengele cha methali.

(b) Walimu waweke msisitizo katika matumizi sahihi ya sarufi na mjengo wa tungo ili kuwajengea wanafunzi weledi katika mada hiyo waweze kuondokana na matumizi ya kisarufi yasiyo sahihi na kuongeza uwezo wa kujieleza kwa ufasaha.

(c) Msisitizo uwekwe katika kusoma vitabu vya ushairi, tamthiliya na riwaya ili wanafunzi wapate maarifa ya kutosha katika vipengele vya fani na maudhui.

(d) Uhamasishaji uwekwe katika utunzi wa kazi za fasihi ili wanafunzi wapate ujuzi na maarifa ya kutosha katika kutunga kazi mbalimbali za fasihi.

(e) Wadau wa elimu, walimu na wanafunzi kwa jumla waweke msisitizo katika ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Kiswahili kikamilifu ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa mada zote.

**KIAMBATISHO A**

## UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

| Na. | Mada | 2018 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 30 au zaidi** | **Maoni** |
| 1. | *Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi* | 12, 13, 14 | 89.5 | Vizuri |
| 2. | *Uandishi* | 8, 9 | 88.6 | Vizurii |
| 3. | *Ufahamu* | 1,2 | 74.3 | Vizuri |
| 4. | *Maendeleo ya Kiswahili* | 10 | 74.3 | Vizuri |
| 5. | *Sarufi* | 3, 4, 5, 6, 7 | 64.1 | Wastani |
| 6. | *Kutunga kazi za Fasihi* | 15 | 58.7 | Wastani |
| 7. | *Fasihi Simulizi* | 11 | 17.7 | Hafifu |

**KIAMBATISHO B**

**ULINGANIFU WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2017/2018**

| Na. | Mada | | 2017 | | 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 30 au zaidi | Maoni | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 30 au zaidi | Maoni |
| 1. | *Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi* | 12, 13, 14 | 82.1 | Vizuri | 89.5 | Vizuri |
| 2. | *Uandishi* | 8, 9 | 85.2 | Vizuri | 88.6 | Vizurii |
| 3. | *Ufahamu* | 1,2 | 87.2 | Vizuri | 74.3 | Vizuri |
| 4. | *Maendeleo ya Kiswahili* | 10 | 34.5 | Wastani | 74.3 | Vizuri |
| 5. | *Sarufi* | 3, 4, 5, 6, 7 | 43.9 | Wastani | 64.1 | Wastani |
| 6. | *Kutunga kazi za Fasihi* | 15 | 70.5 | Vizuri | 58.7 | Wastani |
| 7. | *Fasihi Simulizi* | 11 | 85.5 | Vizuri | 17.7 | Hafifu |

KIAMBATISHO C

**CHATI YA ULINGANIFU WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2017/2018**

